Jumatatu Januari 29, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • No. 0581570
www.ippmedia.com
MWANGA WA [illegible]

LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_new[illegible]



**XAVI KUJIUZULU BARCELONA JULAI**

UKURASA 22

**MAKONDA** amwaga machozi kisa mama kudhulumiwa ardhi



UKURASA 2

**MISWADA** sheria uchaguzi, umeme kutikisa bungeni

UKURASA 4

**WIZARA,** NMB waingia mkataba kuinua uchumi wa kidigitali

UKURASA 8

# Wafanyabiashara watekwa wakiwa kituo cha mafuta

**WATEKAJI** watumia cruiser nyeupe, maswali ya ndugu yakosa majibu polisi...

*Endelea ukurasa wa 2*



Juma Mwiru



Haruna Mwiru




Godbless Lema


# Lema: Nitagombea ubunge 2025 nipate thawabu kwa Mungu

UKURASA 3

UKURASA WA 23

## MWAKINYO AMCHAPA MGHANA KWA KO SASA AMTAKA KIDUKU

BAADA ya Bondia wa Ngumi za Kulipwa nchini, Hassan Mwakinyo, kushinda Mkanda wa Ubingwa wa WBO Afrika, kwa kumchapa Mghana Elvis Ahorgah kwa KO katika raundi ya saba kwenye pambano la raundi 10 uzani wa Super Middle, lililopigwa Indoor New Amaan Sports Complex mjini Zanzibar usiku wa kuamkia jana, amesema sasa anamtaka Twaha Kiduku ulingoni ili kumaliza...



## Sare, madaftari vyawakwamisha wanafunzi 4,000 kuripoti sekondari

UKURASA 3

**MICHEZO** SERENGETI GIRLS YATAKA KUFANYA KWELI ZAMBIA UK. 23 **KATUNI** UK. 6

# Makonda amwaga machozi ziarani

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa**
SHINYANGA

MGOGORO kati ya mwekezaji na mwananchi wa kawaida, Nyangeta Malawa, umemtoa machozi Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, akiwa ziarani mkoani Shinyanga.

Baada ya kupewa taarifa kuhusu kinachoendelea dhidi ya mwananchi huyo, Makonda alijikuta akibugujikwa machozi na kujikuta aimba tenzi za rohoni, akishindwa kuzungumza na kuamua kushuka jukwaani.

Hiyo ilikuwa wilayani Kahama. Makonda akiwa Kata ya Tinde wilayani Shinyanga, mama huyo aliyelazimika kumfuata mwenezi huyo kusaka utatuzi wa kero yake, alipatiwa kipazasauti, akadai kupokwa eneo lake na mwekezaji wa kiwanda cha unga wa mahindi.

Makonda alisema "baba wa watu (mume wa mama huyo) haonekani na hukumu zipo. Hivi RPC (Mkuu wa Polisi Mkoa) yupo wapi? Aje atupatie majibu."

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, alisema anakumbuka tukio hilo la kupotea wakiwa katika baraza la kata, Jeshi la Polisi walifungua kesi na kuipeleka kwa mwanasheria.

Alisema wakati hati ya mashtaka inatoka, mwekezaji huyo alilalamika kwenye mamlaka kubwa zaidi - Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP). Jalada likapelekwa huko.

Makonda alihoji muda wa jalada hilo, akijibiwa na kamanda huyo kuwa lina zaidi ya miezi mitatu.

"Tangu mtu amepotea ana miaka mitatu halafu jalada lina miezi mitatu?" Makonda alihoji na kujibiwa na Kamanda Janeth kuwa "ni kweli tukio lina miaka mitatu tangu mtu amepotea na tunafuatilia Ofisi ya Mwanasheria."

Makonda alieleza kusikitishwa na hali hiyo, akiimba wimbo toka tenzi za rohoni "Bwana Mungu ninashangaa kabisa..."

Awali mama huyo alidai "mume wangu ametekwa siku ya usuluhishi wa Baraza la Ardhi na barua zote ninazo na mtuhumiwa ambaye tunamtuhumu amemteka mume wangu mwaka 2021 wamekuja kujenga kiwanda kwenye eneo la mume wangu.

"Ninaomba Makonda unisaidie, huyu mtu ni maarufu Kahama ana shule zake binafsi. Sisi anatuonea."

Makonda baada ya kumsikiliza alihoji "kwa hiyo, haki ya hukumu ya ardhi kutoka Baraza la Ardhi inaonesha ni ya mume wako? Kwa hiyo, watu wa serikali wamekaa kimya, ardhi haijarudi na mume hajulikani?"

Mama huyo alijibu "ndio, ardhi ni ya mume wangu na mume wangu hajulikani aliko, ametekwa na tuna barua kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) makao makuu ina vielelezo vinaeleza wamebaini mmiliki halali ni mume wangu na nyaraka ya pili ilijulikana ni ya kughushi. Ziliunganishwa na watumishi wa umma, barua hizi hapa ninazo," alidai.

Makonda alisema "sasa ardhi haijarudi na mume kapotea na anayeshtakiwa kaenda kujenga katika hilo eneo na serikali imekaa kimya. Hii si sawa, labda Mkuu wa Mkoa uje utupe maelezo tofauti tuelewe tu, lakini si jambo zuri."

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, alisema suala hilo linashughuliwa na Kamanda wa Polisi Mkoa.

"Sisi maskini tuna kosa gani jamani? Mbona mnatuonea, eneo mmechukua na baba wa watu haonekani na hukumu zipo. Hii si sawa!" Makonda alilalama.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (wa tatu kulia), akiangalia mitambo ya umeme katika kituo cha umeme cha New Pangani (MW 68) kilichoko wilayani Korogwe, mkoani Tanga, ambacho kilisimama kuzalisha umeme kwa zaidi ya wiki mbili. **PICHA: TERESIA NHAGAMA**

ZIKITIMU SIKU 31

# Hofu yatanda wafanyabiashara waliotekwa kituo cha mafuta

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WAFANYABIASHARA wawili wa familia moja, wakazi wa Manispaa ya Singida waliotekwa na watu wasiojulikana.

Ni mwezi mzima sasa wakiwa hawajulikani waliko huku hofu ikiendelea kutanda kwa ndugu na jamaa kama wako hai au wameuawa.

Wafanyabiashara hao wanaodaiwa kutekwa katika Manispaa ya Singida Desemba 28, mwaka jana, ni Juma Mwiru ambaye ana ofisi eneo la Mitunduruni na Haruna Mwiru, mmiliki wa kiwanda cha kuchana mbao kilichoko Unyankindi, Manispaa ya Singida.

Mmoja wa wanafamilia mwishoni mwa wiki aliwasilisha ombi kwa Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Paul Makonda, akiomba chama kiingilie kati ili ndugu zao waliotekwa wapatikane.

"Mume wangu alitekwa tangu Desemba 28, 2023 akiwa na shemeji yangu. Tumekwenda Kituo Kikuu cha Polisi, kwa RPC na kwa Mkuu wa Mkoa, lakini bado hawajapatikana hadi sasa.

"Nina watoto saba pamoja na wa shemeji yangu wanashindwa hata kwenda shuleni, hali ya maisha ni ngumu," alilalama Mwanahamis Sombi, mke wa Haruna Mwiru.

Kutokana na malalamiko hayo, Makonda alimwita Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Singida, Moses Machali ambaye alisema ofisi ya Mkuu wa Wilaya inalifahamu tukio hilo na ilishaagiza Jeshi la Polisi kuchunguza kubaini waliko wafanyabiashara hao.

"Ni kweli watu hao walipotea katika mazingira ya kutatanisha, waliaga wanakwenda kazini, lakini baada ya hapo hawakurudi nyumbani hadi sasa. Tumeliagiza Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi ambao unaendelea hadi sasa," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema mama huyo (Mwanahamis Sombi) alifika ofisini kwake mara mbili kutoa taarifa ya tukio la kutekwa mume wake pamoja na shemeji yake.

Alisema baada ya kupewa taarifa hizo, alimshirikisha Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Stella Mutabihirwa ambaye naye alimshirikisha Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP). Sasa Jeshi la Polisi katika vituo vyote nchini linaendelea na uchunguzi wa tukio hilo.

Makonda alisema kwa kuwa suala hilo ni la jinai, alimwuliza mkuu wa mkoa serikali "itamwachaje" mama huyo ambaye watoto wake hawaendi shuleni kutokana na hali ngumu ya kimaisha baada ya kutekwa baba zao, Serukamba aliahidi kuwa ofisi yake itampatia mama huyo Sh. milioni mbili Jumatatu (leo) zimsaidie.

**WALIVYOTEKWA**

Hassan Juma ambaye ni mtoto wa Juma Mwiru aliyetekwa, alidai watekaji walifika katika kituo kimoja cha kuuza mafuta (jina tunalihifadhi) kilichoko Mwenge wakiwa kwenye gari jeupe aina ya Toyota Cruiser.

Alidai kuwa gari hiyo baada ya kufika katika kituo hicho cha mafuta, walishuka watu wawili na kumchukua baba yake mdogo Haruna Mwiru (aliyetekwa) na kuondoka naye kwenda kusikojulikana. Gari liliondolewa eneo hilo kwa kasi.

Alisema kuwa baada ya tukio hilo, alianza kutoa taarifa kwa ndugu na jamaa kuwajulisha kilichotokea ndipo taarifa zikapelekwa hadi Kituo Kikuu cha Polisi Singida kulikofunguliwa jalada la uchunguzi.

Omari Mwiru alidai alipigiwa simu saa 11:48 jioni na Juma Mwiru (aliyetekwa) na kumweleza kuwa amepata dharura kwa siku mbili hadi tatu hatakuwapo mjini.

"Alivyonipigia simu akaniomba niende nyumbani kwake nikachukue funguo za gari ili nikaichukue kuipeleka kwake iko sheli (kituo cha mafuta) na kwamba nikamchukue mjomba maana shemeji yake, yaani mke wa Juma Mwiru yuko safarini Mwanza.

"Akaendelea kunieleza kuwa kama kutakuwa na changamoto yoyote ya fedha nijiongeze, nikamwuliza kwani kuna shida, hakujibu na baadaye nilipompigia tena kumwuliza simu yake ikawa haipatikani," alidai.

Sakina Hamis ambaye ni mke wa Juma Mwiru (aliyetekwa) alidai alipigiwa simu na mume wake saa 11:05 jioni, lakini alipoanza kuongea, ghafla alimtaka asubiri kidogo, akiahidi angempigia tena.

Alidai kuwa baadaye ilipofika saa 12 jioni, alimpigia tena mumewe huyo, lakini simu yake ikawa haipatikani na hivyo kuamua kuwapigia simu watoto kuwauliza kama baba yao alikuwa nyumbani.

"Nilipowapigia simu watoto waliniambia baba yao hakuwa nyumbani ila baba mdogo alikwenda nyumbani akawapelekea fedha kwa ajili ya matumizi na kwamba baba yao (aliyetekwa) atakuwa nje ya mji kwa siku mbili hadi tatu.

"Nilipata wasiwasi mkubwa, nikampigia simu shemeji yangu Omari kumwuliza kama kuna tatizo lililokuwa limetokea," alidai.

Ndugu mwingine Seif Mwiru alisema wameshatoa taarifa katika vituo vyote vya polisi mkoani Singida, kwa Kamanda wa Polisi Mkoa na Mkuu wa Mkoa lakini hawajawapata ndugu zao.

Abdallah Mkoko ambaye ni Diwani wa Mitunduruni alisema tukio la kutekwa wafanyabiashara hao linaichafua taswira ya nchi kwa kuwa hawana historia ya uhalifu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, ACP Stella Mutabihirwa alisema jeshi hilo lina taarifa za kupotea kwa wafanyabiashara hao na jalada la uchunguzi limefunguliwa.

HABARI KITAIFA

## Sare, madaftari vyakwamisha wanafunzi kuripoti sekondari

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

ZAIDI ya wanafunzi 4,000 kati ya 6,300 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wilayani Masasi mkoani Mtwara hawajaripoti kutokana na sababu mbalimbali.

Sababu hizo zinatajwa ni wazazi kukosa mahitaji ya msingi yakiwamo madaftari, sare na viatu.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Louter Kanoni wakati akifungua mafunzo ya matumizi ya takwimu za sensa ya watu na makazi kwa watendaji na viongozi mbalimbali kutoka wilaya za Newala, Masasi na Nanyumbu, hali hiyo sio ya kuridhisha.

Alisema kuna kundi kubwa la wanafunzi halijaripoti shuleni kuanza masomo ya kidato cha kwanza, huku akiwataka Watendaji Kata kushirikiana na vijiji na mitaa kuwafuatilia wazazi na walezi wa watoto hao.

Alisema Wilaya ya Masasi kwa halmashauri zote mbili imefaulisha zaidi ya wanafunzi 6,000 na wote kutakiwa kuripoti shuleni ili kuanza masomo, lakini hali hairidhishi kutokana na idadi ndogo iliyoripoti.

"Tumefanya ziara ya kukagua wanafunzi walioripoti takribani wiki nzima katika baadhi ya shule zetu ili kuona hali ya uripoti kwa wanafunzi hao kwa kweli ni mbaya sana wanafunzi zaidi ya 4000 kati ya 6300 bado hawajaripoti shuleni," alisema Kanoni.

Ofisa Elimu Sekondari Halmashauri ya Mji Masasi, Elitrida Mtewele, alisema idadi ya wanafunzi walioripoti kidato cha kwanza sio ya kuridhisha, huku akiitaka jamii kushiriki kuhamasisha umuhimu wa elimu.

"Tunaendelea kuwahamasisha wazazi na walezi ili wanafunzi wote ambao wamefaulu kwenda sekondari wanakwenda shuleni kuripoti, lakini tunatoa wito kwa jamii kuwa elimu ndio urithi kwa mtoto na kila anayepaswa kwenda shule aende shuleni haraka ili akaanze masomo," alisema.

Alisema maofisa elimu kata, watendaji wa vijini na mitaa tayari wameshepewa maagizo kuwa wahakikishe watoto wote waliofaulu kwenda sekondari wanakwenda kuanza masomo.

Athumani Bakari, mmoja wa wazazi ambaye mtoto wake amefaulu, lakini hajaripoti shuleni alisema anashindwa kuripoti shuleni kwa sababu hajafanikiwa kupata fedha za kumnunulia mahitaji ya msingi ya shuleni ikiwamo sare, viatu na madaftari kwa kuwa hali ya kipato ni ngumu.

Adija Saidi, aliunga mkono kuwa hali ya uchumi kwa wazazi na walezi ni ngumu ndio sababu baadhi ya wanafunzi kushindwa kuripoti shuleni, lakini wazazi wana upendo na watoto wao watakapaofanikiwa kupata fedha watawapatia mahitaji ya msingi na watakwenda shuleni.



Mkandarasi na viongozi mbalimbali wa serikali wakiangalia eneo ambalo kunatarajiwa kuanza ujenzi wa bandari ya Mbamba Bay, Nyasa mkoani Ruvuma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Lema: Nitagombea ubunge nipate thawabu kwa Mungu

**Na Elizabeth Zaya**

MBUNGE wa zamani wa Arusha Mjini, Godbless Lema, amesema mpango wake wa kugombea ubunge katika uchaguzi ujao si kwa ajili ya kazi hiyo kumpatia kipato bali kufanya kazi hiyo ili apate thawabu kwa Mungu kwa kupigania haki za watu.

Lema ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Kaskazini, amesema kipato kitokanacho na kazi ya ubunge ambacho ni kati ya Dola 5,000 au 6,000 (Sh. milioni 12 au milioni 15) ni fedha ndogo na huo si mshahara wa mtu aliye kwenye daraja la kati kiuchumi. Alisema hayo jana wakati wa mahojiano kwenye kipindi cha medani za siasa kinachorushwa na Star Tv.

"Sipiganii haki nikawe mbunge, nilipwe mshahara. Mshahara wa mbunge ni dola 5,000 au 6,000, huo sio mshahara wa mtu ambaye yuko kwenye 'middle income class' (kipato cha mtu daraja la kati), ni hela ndogo sana, ni kima cha chini cha mshahara wa mtu anayefanya kazi North America (Amerika ya Kaskazini) au anayefanya kazi Europe (Ulaya) ambayo imeendelea," alisema Lema.

"Actually (kwa kweli), wabunge wanaonekana wana hela kwa sababu wanakaa katikati ya kundi kubwa la watu maskini, lakini vinginevyo wabunge ni maskini sana. Ndio maana akija hapa Dar es Salaam anatafuta hoteli ya elfu 20. Akilala hoteli ya laki moja, laki mbili lazima apate shambulio la moyo sababu haiendani na posho. Kwa hiyo mimi sipambanii kuwa mbunge kwa sababu ubunge ni ajira inayonipa biashara."

Alisema huwa anajisikia vibaya jitihada zake za kutetea watu zinapohusishwa kuwa ni kwa ajili ya kutaka ubunge.

"Ngoja nikusaidie...mimi ni Mchaga...yaani siku nikianza kuwaza kwamba eti nigombanie ubunge kwa ajili ya dola 5,000 au 6,000 kila mwezi halafu mke wangu na watoto wangu wakajua hayo ndio mawazo yangu ah... nilikuwa natumia fedha za ubunge kama ujira wangu, lakini sio fedha ya maana. Inakuwa ya maana kwa sababu wabunge wameshindwa kupigania ustawi wa watu wengine kama mwalimu na daktari," alisema Lema.

"Mwalimu angekuwa analipwa dola 1,500 mpaka 2,000 au polisi wa chini anayepigwa upepo usiku kulinda raia angekuwa analipwa Shilingi milioni tatu, au nesi angekuwa analipwa Shilingi milioni nne au tano asingeona Sh. milioni 12 au milioni 15 ya mbunge ni kubwa," alisema Lema.

Alisema endapo polisi angekuwa analipwa Sh. 100,000 ya posho anapofanya kazi za usiku asingeona posho anayolipwa mbunge anapokaa kwenye vikao vya bunge ni kubwa akisema inaonekana hivyo kwa sababu wabunge wameshindwa kutetea maisha ya watu wengine.

"Mwalimu analipwa Shilingi lakini nne, kwa hiyo kwa mwaka mshahara wake ni Sh. milioni 4.8. Mshahara wa mbunge kwa mwezi labda ni Sh. milioni 15, kwa hiyo mashahara wa mwalimu wa miaka mitatu ni mshahara wa mbunge wa mwezi mmoja, kwa hiyo 'crisis' (msuguano) inaanzia hapo. Watu wanaona mbunge analipwa kifisadi wakati ni hela ya kawaida sana kulingana pia na majukumu yake isipokuwa ameshindwa kujali maslahi ya watu wengine waishi vizuri."

Kadhalika, alisema jambo la msingi linalotakiwa kufanyika sio mbunge kupunguziwa maslahi yake bali ni mbunge huyo kuona kwamba kama anafikia anaona Sh. milioni 12 haitoshi akaomba mshahara wake uongezeke hadi Sh. milioni 18 anaonaje ni sawa polisi ashinde kwenye upepo usiku kulinda usalama wa raia halafu alipwe Shilingi laki sita kwa mwezi.

"Ina maana hajali ubinadamu. Mbunge anayejali ubinadamu atapiga kelele mishahara iongezwe kwa wafanyakazi wote na wakawa na fursa ya mikopo kama ilivyo kwa wabunge. Angepigania maisha hayo kwa wananchi, hakuna ambaye angesema analipwa hela nyingi, inaonekana wanalipwa nyingi kulingana na jamii kubwa wanakotoka namna inavyolipwa," alisema.

Alisema asilimia 90 ya wabunge wa sasa hawajui kazi ya ubunge.

"Tafuta hotuba zangu bungeni, sijawahi kuomba mitaro ndani ya bunge. Wabunge wa sasa hivi ukiwaona wanatoa zawadi sijui za mbuzi, sijui wana kombe la nini. Mimi nilikuwa naongea vitu ambavyo vinafanya 'mindset transformation'. Ukisimama kuongelea biashara, umefanya utafiti na umechambua. Kazi ya mbunge ungeiona bungeni akiongelea mfumuko wa bei au hakuna umeme," alisema.

Kuhusu kugombea ubunge Arusha Mjini katika uchaguzi ujao, alisema, atagombea na ana uhakika atashinda kwa asilimia 95.

"Nikichukua fomu na nigombanie ubunge Arusha Mjini na nitagombania, Nitapata asilimia 95 na naweza nisifanye kampeni kabisa...nawajua watu wangu na watu wangu wananijua. Labda niseme hivi...kungekuwa na ruhusa ya mtu mmoja kugombania majimbo matatu, ningeshinda kwa sababu najua namna ya kuwaambia watu na watu wananijua si Arusha pekee," alijingamba.

Kuhusu jimbo hilo la Arusha, alisema tayari alishamwambia mbunge wa sasa atunze fedha zake vizuri pamoja na kiinua mgongo maana hawezi kuwa mbunge tena wa jimbo hilo na ikiwezekana anaweza kumwajiri.

Alipoulizwa kuhusu deni alilokuwa akidaiwa alilokopa wakati akiwa mbunge, Lema alikiri kwamba alikuwa anadaiwa deni kubwa, lakini alilipa lote na hadaiwi chochote.


## NAFASI YA KAZI

KAMPUNI YA MADAWA ILIYOPO DAR ES SALAAM INATAFUTA MTU WA MAUZO AWE MWANAMKE AU MWANAUME.

PIGA SIMU NAMBA: +255 713 786 300



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Jenista Mhagama (katikati), akiangalia upanuzi na ukarabati wa daraja la Kunduchi jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki baada ya maji ya mvua kuharibu daraja hilo. **PICHA: MURAJI MSALA**

# Miswada waliyoikataa CHADEMA, umeme, sukari kutikisa bungeni

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MKUTANO wa 14 wa Bunge unaanza vikao vyake kesho jijini Dodoma huku wabunge wakitarajiwa kujadili masuala mbalimbali ikiwamo miswada ya sheria za uchaguzi na siasa ambayo imesababisha maandamano ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Hiyo ni miswada ya: Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, 2023; Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, 2023; na Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa, 2023.

Ilisomwa kwa mara ya kwanza katika Bunge la Novemba mwaka jana na baada ya hatua hiyo ilipelekwa kwenye Kamati ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kwa ajili ya kuchambuliwa na kupokea maoni ya wadau.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dk. Joseph Mhagama, alisema kamati iko hatua za mwisho kukamilisha uchambuzi wa maoni ya wadau na baada ya kukamilisha itawasilisha bungeni.

Dk. Mhagama alisema kamati hiyo ilikaa kwa siku nne kupokea maoni ya wadau 1,707. Ni idadi kubwa zaidi ya wadau kujitokeza mbele yao. Haikuwahi kutokea na wanaamini itachukua muda mrefu kujirudia.

"Tunaelekea kumaliza kuchambua na miswada itakwenda bungeni mara Bunge litakapoanza vikao vyake wiki ijayo," alisema.

**YALIYOMO**

Hoja zilizomo katika miswada hiyo ni pamoja na muundo mpya wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) utakaokuwa na kamati maalum itakayosaili wajumbe na Mkurugenzi wa Uchaguzi.

Muswada unapendekezwa kufutwa utaratibu wa kupita bila kupingwa kwa mgombea na badala yake atapigiwa kura ya ndiyo au hapana na atakuwa amechaguliwa kihalali kuwa mbunge endapo atapata kura nyingi za ndiyo kati ya kura zote halali zilizopigwa.

Pia inapendekezwa kila chama cha siasa kuwa na sera ya jinsia na ujumuishi wa makundi maalum na maandamano ya vyama vya siasa yatafanyika kwa kuzingatia Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi na muswada umeainishwa utaratibu wa kuzingatiwa kabla na wakati wa kufanya maandamano au mikutano.

Katika Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023, inapendekezwa kuwa Kamati ya Usaili itapokea na kufanya uchambuzi wa maombi ya watu wanaoomba kuteuliwa kuwa wajumbe wa tume hiyo na kupendekeza majina ya watu wenye sifa kwa Rais kwa ajili ya uteuzi na mjumbe atatumikia nafasi hiyo kwa miaka mitano.

Inapendekezwa kuwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa tume hiyo ya uchaguzi watateuliwa na Rais kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 74 ya Katiba na watapaswa kuwa majaji wa Mahakama Kuu au ya Rufani au kuwa na sifa ya kuwa wakili na wamekuwa na sifa hizo kwa zaidi ya miaka 15.

Sheria hiyo inayopendekezwa inaweka utaratibu wa Rais kuunda kamati ya uchunguzi endapo anaona inafaa, ambayo itafanya uchunguzi na kumshauri ipasavyo kuhusu kuondolewa mjumbe wa tume hiyo ya uchaguzi.

Inapendekezwa pia kwamba tume itakuwa chombo huru na kinachojitegemea na uamuzi wake hautaingiliwa na chombo chochote au kulazimika kufuata maagizo ya mtu yeyote au idara yoyote ya serikali au maoni ya chama chochote cha siasa.

Kama sheria hiyo itapitishwa na Bunge, kutakuwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi atakayeteuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na tume na atakuwa na sifa ambazo ni: raia wa Tanzania wa kuzaliwa, mtumishi wa umma mwandamizi, mwaminifu na mwadilifu na ambaye hajawahi kushika nafasi ya madaraka ya juu katika chama chochote cha siasa.

Muswada unaweka masharti kwamba mtu yeyote atakayekuwa anatekeleza majukumu ya tume atachukuliwa kuwa mtumishi wa tume kwa kipindi chote atakachokuwa anatekeleza majukumu hayo na atapaswa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni za utekelezaji wa majukumu ya tume.

Kadhalika, inapendekeza kuondolewa sharti la vyama vya siasa kuwasilisha stakabadhi halisi za matumizi ya gharama za uchaguzi kwa Msajili wa Vyama vya Siasa ili stakabadhi hizo zibaki kwenye vyama kwa ajili ya kuwasilishwa kwa mkaguzi.

Kwenye marekebisho hayo kumewekwa adhabu chama cha siasa kitakachomruhusu asiye raia wa Tanzania kushiriki katika mchakato wa kufanya uamuzi ndani ya chama husika. Lengo ni kukomesha vitendo vya wasio raia kuingilia uamuzi ya vyama vya siasa kwa kuwa sheria ya sasa inaweka katazo bila adhabu.

Pia inapendekezwa kuondolewa takwa la wagombea kuwasilisha taarifa kuhusu timu ya kampeni kwa Mkurugenzi wa Halmashauri, Katibu Tawala wa Wilaya na Ofisa Mtendaji Kata na badala yake ziwasilishwe kwa Msimamizi wa Uchaguzi na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

Marekebisho mengine ni kuboreshwa utaratibu wa kuchukua na kuwasilisha fomu za tamko la gharama za uchaguzi ili fomu zichukuliwe kwa msimamizi wa uchaguzi wakati mtiania anachukua fomu za kuomba uteuzi na kuwasilishwa wakati wa kurejeshwa fomu za uteuzi.

Lengo ni kutoa muda wa kutosha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kupitia taarifa zinazowasilishwa na watia nia kuhusu gharama wanazokusudia kutumia katika uchaguzi kabla hawajaanza shughuli za kampeni.

Inapendekezwa pia kutungwa Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2023 ambayo inakusudia kuunganisha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa.

Hatua hiyo inalenga kurahisisha usimamizi na utekelezaji masharti yote ya sheria hizo ambazo hutekelezwa na mamlaka moja ambayo ni Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

**WANACHOPINGA WADAU**

Baadhi ya mabadiliko yanayopingwa katika miswada hiyo ni pamoja na muundo wa kamati inayochagua makamishna wa Tume ya Uchaguzi, pia uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa tume ya uchaguzi kufanywa na Rais ambaye ni mwenyekiti wa chama tawala.

Vyama vya upinzani vinataka Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa tume wachujwe na kuchaguliwa na kamati huru.

Mathalani, CHADEMA inadai kuwa miswada hiyo "ni mibaya sana", hakuna haja ya kuifanyia marekebisho. Wanataka iondolewe na iandikwe upya kabisa.

Kwa sasa, chama hicho kinataka serikali iwasilishe muswada wa kutunga Katiba mpya na mwingine kwa marekebisho ya Katiba ya sasa ya mwaka 1977.

Mbali na miswada hiyo, Bunge pia litapokea na kujadili taarifa mbalimbali za kamati za Bunge ambapo mambo mengine yanayotarajiwa kuibua mjadala mkali ni pamoja na uhaba wa sukari nchini, umeme wa ratiba,

## TCRA yajivunia mfumo mpya wa mawasiliano kwa watoa huduma

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imesema huduma za mawasiliano kwa watoa huduma zimerahisishwa baada ya kukamilika mfumo wa Tanzanite Portal unaoleta pamoja watoa huduma wakubwa na wadogo.

Mjini Unguja, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, alisema mwishoni mwa wiki kuwa mfumo huo unaowezesha mamlaka hiyo kutoa huduma mbalimbali kwa wateja wake ambao ni watoa huduma za mawasiliano nchini, ikiwamo kuwezesha usajili wa bidhaa na huduma za sekta ya mawasiliano, utoaji leseni na ulipaji tozo.

"Tumeongeza ufanisi katika kuhudumia mteja kupitia dirisha moja la maombi ya leseni za aina zote, utoaji vyeti vya uhakiki wa vifaa vya kielektroniki, kanzidata ya anuani za makazi na dawati la huduma kuwezesha mawasilisho ya malalamiko ya wateja," alisema.

Dk. Jabiri alisema mfumo huo unawezesha uwasilishaji maombi ya leseni na nambari za mawasiliano bila mwombaji kufika kwenye ofisi za TCRA.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, mfumo huo unawezesha upangaji, ugawaji na ufuatiliaji postikodi za anwani za makazi; ushughulikiaji wa maoni, changamoto na taarifa mbalimbali kutoka kwa wateja wa TCRA ambao ni watoahuduma za mawasiliano nchini.

Mfumo huo pia alieleza unaiwezesha TCRA kubainisha leseni za watoa huduma, kupata taarifa za watoa huduma kiurahisi zaidi pamoja na kuwezesha mamlaka hiyo kupata taarifa za malipo za watoa huduma za mawasiliano. Aliongeza kuwa mfumo huo pia unarahisisha ushughulikiaji maombi ya uhakiki wa vifaa vya kielektroniki na kumwezesha mwananchi au mwenye leseni ya mawasiliano kukamilisha uhakiki wa leseni za mawasiliano kwa kutumia simu ya mkononi kupitia msimbo wa USSD *150*52#.

Alisema msimbo huo unamwezesha mwananchi kuhakiki uhalali wa huduma zinazotolewa na mtoa huduma, ili kuhakikisha kunakuwapo udhibiti wa watoahuduma za mawasiliano wasioidhinishwa na mamlaka hiyo iliyopewa jukumu la kutoa, kuhuisha na kutwaa leseni za mawasiliano nchini.

"Tanzanite Portal umeundwa kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma kwa wadau wote wa sekta ya mawasiliano nchini. Mfumo huu umeunganisha huduma mbalimbali katika dirisha moja, kutoa urahisi na ufanisi zaidi katika mchakato mzima wa huduma za TCRA," alisema.

Wakizungumzia mfumo huo, baadhi ya wadau wa sekta ya mawasiliano, wakiwamo wanaotoa maudhui ya habari kwenye mtandao na wauzaji vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki, walipongeza TCRA kwa kuweka dawati la pamoja la mtandaoni linalowakutanisha na msimamizi huyo wa sekta.

"Mafanikio haya yanathibitisha dhamira ya TCRA katika kuleta mageuzi chanya katika sekta ya mawasiliano, huu mfumo ninaamini utatuondolea usumbufu wa kutumia muda mwingi kufuatilia leseni na masuala mengine pale TCRA, wamesaidia sana kuleta hili jukwaa," alisema Lucas, mmoja wa watoa huduma za mawasiliano nchini.

Chalila Kibuda miongoni mwa wadau wa maudhui mtandaoni, alisema "jukwaa hili kwa jinsi Mkurugenzi Mkuu alivyoelezea litatufaa sana wanahabari wa mtandaoni kushughulikia masuala ya kupata leseni na taarifa, tunawapongeza mamlaka kwa hatua hii muhimu."

# Wanataaluma wataka sera moja usalama wa chakula

**Na Romana Mallya**

WANATAALUMA wa sayansi na teknolojia ya chakula nchini wamesema kuna haja nchi kuwa na sera moja ya usalama wa chakula itakayowaongoza kila mtu kupata chakula salama.

Mwenyekiti wa Chama cha Wataalamu wa Sayansi na Teknolojia ya Chakula (TAFST), Mercy Mmasi, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika mkutano wa mwaka uliojadili masuala ya kitaifa, likiwamo la sera ya usalama wa chakula.

Alisema wameona kuna umuhimu wa kuwa na suala hilo kwa wakati huu kwa sababu utafiti na malengo ya kitaifa na kimataifa, yanaongelea umuhimu wa usalama wa chakula.

"Usalama huo sio tu kwa afya za binadamu bali pia, kwa maendeleo ya nchi, kwa kuwa hupunguza mzigo wa magonjwa na hupunguza upotevu wa chakula kama tunavyojua kuna kasi ya ongezeko la watu duniani.

"Tukiendelea kuchafua chakula au kukipoteza ina maana tutaingia kwenye hatari zaidi. Wataalamu tunaishauri serikali, kutoa maoni katika yale tunayoona yakifanyika yatakuwa na afya kwa ajili ya wananchi na kuleta maendeleo kwa taifa," alisema.

Mercy alisema wamejikita katika sera ya usalama wa chakula kwa kuwa, wanaamini watakapo kuwapo itakuwa mwongozo na kwa vitu vingine.

Alisema takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), inakadiriwa kwamba kila mwaka watu milioni 600 hupata magonjwa na watu 420,000 hufa kutokana na kula chakula kilichochafuliwa. "Tunapoongelea chakula, kinaweza kugeuka kuwa sumu na tumeona mara nyingi, tumesikia watu wamekula samaki aina ya kasa wanakufa, wengine uyoga au mihogo. Vyakula vingine vina sumu ya asili na vingine vinachafuliwa.

"Kuna aina ya vimelea na bakteria ambao wanaweza kuchafua chakula kiasi kwamba, mtu anaweza akafa au kupooza," alisema.

Kutokana na hilo, Mercy alisema TAFST wanatoa elimu kwa jamii kwa njia ya mitandao na midahalo kuhusu chakula salama na kwa mwaka 2023, waliwafikia watu zaidi ya 600.

Pia, alisema wanatoa elimu kuhusu uhifadhi wa chakula, usalama wa chakula na upatikanaji wake. Chama hicho kina wataalamu zaidi ya 600 na watafiti wanaoendelea na utafiti kuhakikisha mambo mengi wanakwenda kugundua.

Kadhalika, wanaendelea kuishauri serikali na wadau wa maendeleo kufahamu ni maeneo gani wanaweza kuwekeza na ni vitu gani wanaweza kufanya ili mwisho wa siku wapate chakula ambacho ni salama.

Wapo tayari kusaidia utaalam na uwelewa walionao ili nchi iwe na sera moja ya usalama wa chakula itakayowaongoza wote, kila mtu apate chakula ambacho ni salama.

Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Uzalishaji Mazao Wizara ya Kilimo, Beatrice Banzi, aliyemwakilisha waziri mwenye dhamana, Hussein Bashe, alisema sera si suala la Wizara ya Afya au Ofisi ya Waziri Mkuu pekee, bali kila wizara ina jukumu la kuhakikisha kunakuwapo na usalama wa chakula.

Mhadhiri Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), Beatha Mkojera, alisema mkutano huo wa wanataaluma wa sayansi na teknolojia ya chakula nchini ni muhimu kwa usalama wa chakula nchini.

Alisema unalenga kuweka mikakati na mipango ambayo watakwenda nayo kwa kasi kuhakikisha wanataaluma wa sayansi ya chakula wanafahamika, wanahamasisha usalama na ubora wa chakula kwa walaji.

"Kauli mbiu ya mwaka huu inasema, "Kama sio salama, sio chakula." Na sisi tuna kaulimbiu; "Chakula bora na salama kwa kila mtu," alisema.

Deorinidei Mng'ong'o kutoka Bodi ya Maziwa Tanzania na mwanachama wa TAFST alisema, jukwaa hilo ni muhimu kwa wataalamu kwa sababu linasimamia misingi ya taaluma na kutoa ushauri serikalini kuhusu usalama wa chakula na lishe na kuwaunganisha pia.

Itakumbukwa kuwa ubora na salama ni nyenzo muhimu katika kufikia malengo ya maendeleo endelevu, hasa malengo namba 1, 2 na 3 yanayohusu kuondoa umaskini, kutokomeza njaa pamoja na kulinda afya ya jamii na ustawi ambayo Tanzania ni moja ya nchi inayoyatekeleza.

Pia mfumo madhubuti wa udhibiti ubora na usalama wa chakula ni ule wenye kukidhi misingi mitano; msingi ya sheria, msingi ya thabiti wa ukaguzi, msingi wa uchunguzi wa kimaabara, msingi wa elimu kwa umma na msingi wa mawasiliano.

Oktoba 16, kila mwaka, Tanzania imekuwa ikiungana na nchi nyingine duniani katika maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani ambayo huratibiwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO).



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (katikati), akimpongeza Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (kushoto), baada ya kusaini hati ya makubaliano ya ushirikiano katika kuinua uchumi wa kidijitali nchini na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Kulia ni Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Mohammed Khamis Abdulla. Habari kamili Uk. 8 **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# BRELA yataja changamoto wananchi kusajili kampuni

**Na Pilly Kigome**

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imetaja changamoto inayowakabili wananchi ni kutokuwa na elimu ya utambuzi wa sheria stahiki za biashara zao kwa kushindwa kutofautisha usajili wa biashara na leseni ya biashara.

Changamoto hiyo inawafanya waingie katika makosa ya kisheria bila kujitambua.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dar es Salaam na Ofisa Leseni, Ndeganka Mbowe wakati wa ufunguzi wa wiki ya sheria iliyoandaliwa na Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam.

Alisema wananchi wengi wanaingia katika makosa ya kisheria kwa kukosa utambuzi huo na kujikuta sheria inawabana kwa kuanzisha viwanda au biashara bila kusajili na kuwa na leseni ya biashara pekee.

Alisema kutokana na hilo wakipitiwa katika ukaguzi wanakabiliwa na makosa ya jinai na kuhisi kama wanaonewa, wanakuwa nyuma ya sheria kwa kuendesha biashara kinyume na utaratibu.

"Sheria ya mwaka1967 inataka unapofanya shughuli yoyote ya kiwanda nchini kiwe kidogo au kikubwa ni lazima ukisajili, kidogo utapata cheti cha usajili na kikubwa utapata leseni ya kiwanda," alifafanua.

Alisema sheria hiyo imegawanywa katika makundi mawili, viwanda vidogo mtaji hauzidi Sh. milioni 100 na viwanda vikubwa na vya kati mtaji wao unazidi Sh. milioni 100 na kuendelea. Mbowe aliwataka wananchi kuyatumia vyema maonesho hayo ya sheria kwenda kupata elimu zinazohusu biashara, ikiwamo kuepukana migogoro ya kisheria. Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, Salma Magimbi, alisema wiki hiyo ya kisheria ina lengo la kuwasiliana na wadau wake moja kwa moja kwa kuongea nao kuwapa elimu ili kupata watu wengi zaidi.

Alifafanua Mahakama iko katika mpango wa maboresho makubwa zaidi ambayo yako katika teknolojia ya TEHEMA ili kuwaambia wananchi hatua zipi wamepiga na kupata fursa kujua zaidi mambo katika kuongea na mahakama.

Kwa mwaka huu wiki ya sheria wamejikita zaidi katika dhana ya haki kwa ustawi wa jamii na taifa, na kuangalia mahakama na wadau katika kuboresha mfumo jumuishi wa haki jinai.

Aidha, alisema wananchi wanatakiwa watambue upatikanaji haki hukumu ni bure haina gharama yoyote ingawa kuna wananchi wengi ambao bado wanadai kusumbuliwa kupata haki yao ya kimsingi kwa kudanganywa na kutapeliwa kutoa fedha ili wasomewe hukumu zao.

# Hospitali Magu yajipanga kudhibiti vifo wajawazito

**Na Christina Mwakangale,** MAGU

HOSPITALI ya Wilaya ya Magu, mkoani Mwanza, imeweka lengo la kudhibiti vifo vitokanavyo na uzazi kwa kuhakikisha hakuna wajawazito wanaojifungulia nyumbani.

Takwimu za wilaya hiyo zinaonesha kwa kipindi cha miaka mitatu vilitokea vifo 11 vitokanavyo na kujifungua, huku mwaka 2021 kati ya waliojifungua 18,468 vifo vilikuwa vinne, mwaka 2022 vinne kati 19,290 waliojifungua na 2023 vifo vitatu kati ya 19,721.

Kaimu Mganga Mkuu hospitali hiyo, Eusebius Chanjali, aliyasema hayo jana, wilayani hapa, mbele ya maofisa kutoka Wizara ya Afya, TAMISEMI na waandishi wa habari, waliokuwa kwenye ziara ya kubaini mafanikio ya Mfuko wa Afya wa pamoja nchini (Health Basket Fund-HBF) kwa kipindi hicho.

"Wanaojifungua hospitalini hapa ni 300 kwa mwezi. Tumejihakikishia hakuna mama anayejifungulia nyumbani ili kuondoa kabisa vifo vya kinamama. Idadi ya vifo imepungua kutoka digiti mbili mwaka 2019 ambavyo vilikuwa zaidi ya 20, sasa vifo ni digiti moja.

"Tunajitahidi kwa uboreshaji huu wa huduma za afya, tutafuta kabisa vifo vya uzazi, haiwezekani mama anayeleta kizazi duniani apoteze maisha kwa sababu ambazo zingeepukika," alisema.

Alisema halmashauri ya wilaya hiyo imepokea zaidi ya Sh. bilioni 5.4 kwa kipindi cha 2021/22-2022/23, ili kuboresha huduma za afya, ikiwamo vituo vya afya, zahanati na Hospitali ya Wilaya ya Magu pamoja na ununuzi wa vifaa tiba na dawa.

Baada ya kuboreshwa kwa huduma za afya, hospitali hiyo imepunguza kutoa na kupokea idadi ya rufani kwa wagonjwa wa dharura, ambao awali walifikishwa Hospitali ya Rufani Bugando na Sekou Toure.

"Rufani labda ziwe za kibingwa, lakini kwa sasa huduma za dharura tunafanya wenyewe hasa upasuaji kwa kinamama wanaojifungua. Tumepunguza matumizi ya hospitali yetu kwa magari ya wagonjwa, ambayo yalihitaji mafuta ili kusafirisha wagonjwa," alisema Kaimu Mganga Mkuu.

"Awali, tulipokea rufani nyingi kutoka vituo vya afya kuja hapa hospitali ya wilaya, kuboresha kwa vituo hivyo kumesaidia kumudu baadhi ya huduma kama upasuaji, kwa sasa tunafanya wenyewe katika vituo vya afya vilivyoboreshwa," aliongezea.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF itoe mapema uamuzi mechi Simba Queens, JKT Queens

**MWANZONI** mwa mwaka huu ilikuwa ichezwe mechi ya Ligi Kuu ya Soka Wanawake kati ya JKT Queens na Simba Queens, lakini haikufanyika kwani kila timu ilienda kwenye uwanja wake.

JKT Queens ilikwenda Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo ambao waliamini kuwa ndiyo ungetumika kwenye mechi hiyo wakati siku hiyo hiyo ya Januari 9, na muda huo huo, Simba Queens ilitinga Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam ambako wao walitaarifiwa kuwa mechi hiyo ingepigwa hapo.

Kilichoonekana ni kwamba waamuzi waliopangwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), walikuwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, huku Meja Jenerali Isamuhyo kukiwa na wachezaji wa JKT Queens peke yao.

Baada ya taratibu zote, waamuzi waliuvunja mchezo huo, hata hivyo, TFF hawakutaka kutoa ufafanuzi sana katika tukio hilo, lakini uongozi wa JKT Queens kupitia kwa msemaji wao, Masau Bwire, alisema walifuata maelekezo ya shirikisho hilo, huku akisema barua ya kubadilisha uwanja ilichelewa kuwafikia ambapo waliipata siku moja kabla ya mchezo kitu ambacho ni kinyume kikanuni.

Hata hivyo ukiangalia kwenye kurasa rasmi za mitandao ya TFF, mechi hiyo ilipaswa kupigwa, Uwanja wa Azam Complex.

Mpaka sasa mechi hiyo haijachezwa tena, timu zinaendelea kucheza raundi zinazofuata za Ligi ya Wanawake Tanzania, lakini kwa jinsi msimamo unavyoonyeshwa na TFF inaonyesha kuwa mechi hiyo haikuwapo. Yaani si kama vile ambavyo baadhi ya watu walifikiria kuwa Simba Queens ilipewa ushindi wa alama tatu na mabao matatu.

Tayari kwa jinsi ligi hii inavyoendelea mpaka raundi ya tisa tu, inaonyesha Simba Queens na JKT Queens wanaendelea kufukuzana kwenye mbio za ubingwa kama ilivyokuwa msimu uliopita, maafande walipotwaa ubingwa huo kwa pointi moja zaidi.

Kwa mtazamo wetu inaonekana msimu huu pia inaweza kutokea mbio kama hizo, kwani timu hizo zinaonekana kuendelea kutawala Ligi ya Wanawake nchini, jambo linalotufanya kuamini kuwa inawezekana kabisa mechi baina yao kuamua bingwa wa msimu huu.

Kwa mantiki hiyo, tunaona ni vema TFF ikajiondoa mapema kwenye lawama itakayokuja kuipata mbele ya safari kwa klabu moja wapo kati ya hizi, au zote mbili kutokana na kutokutoa uamuzi wa mechi hiyo mapema.

TFF Kutofanya uamuzi wa mechi hiyo ni kujitengenezea bomu ambalo viongozi wa shirikisho hilo watahitaji nguvu ya ziada kulitegua.

Ni vema sasa TFF ingeanza kwa kutamka kama mechi hiyo itarudiwa au Simba Queens inatapa ushindi wa mabao matatu na pointi tatu dhidi ya JKT Queens kushindwa kutokea kwenye uwanja ambao mamlaka iliuteua ili uonyeshwe kwenye televisheni.

Na kama utarudiwa, basi ifanye hivyo mapema na si kusubiri hadi mwisho kwani itaonekana kama yenye maamuzi juu ya mustakabali wa ubingwa ni wao.

Inaonekana ni kama TFF inakwepa lawama pande zote mbili kwa kushindwa kusimama au kuamua upande mmoja, badala yake imekaa kimya kwa hili, huku likiwakereketa baadhi ya mashabiki na wadau wa soka.

Ni imani yetu sasa suala hili litafanyiwa kazi haraka ili lisiitie doa TFF na soka la wanawake kwani baadaye inaweza kutafsiriwa kuwa kuna timu inatafutiwa ubingwa na hata ukija ufafanuzi utakaojaa kapu zima itakuwa ni kazi bure tu.

Katika hili sisi tunaona ni kazi ndogo tu, nayo ni kutangaza kama mechi itarudiwa au la. Na kama ni kurudiwa iwe mapema iwezekanavyo ili hili liishe na kila timu iendelee na mechi zake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Wachezaji Tanzania kujifunza AFCON sawa, waamuzi nao?

**NIMEONA** mijadala mingi ya mashabiki wa soka sehemu mbalimbali wakiwataka baadhi ya wachezaji wa Kitanzania kujifunza kwa kile kinachoonyeshwa na wachezaji wa mataifa mbalimbali, hasa yale ambayo yalionekana hayajaendelea sana kisoka.

Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) zinazoendelea nchini Ivory Coast zitabaki kwenye kumbukumbu ya mashabiki wa soka si Tanzania tu, bali Afrika nzima na duniani, kwani zimekuwa na mageuzi makubwa, hii ni baada ya wale mapapa wakubwa waliokuwa wanawameza wadogo, sasa wanamezwa wao.

Zile zama za kuogopa majina makubwa kama Cameroon, Nigeria, Senegal, Misri, Algeria, Morocco, Tunisia, Ghana sasa zimekwisha na badala yake tumeshuhudia nchi ambazo hazikudhaniwa kama zinaweza kuleta ushindani, zikifanya makubwa. Nchi kama Cape Verde, Equatorial Guinea, Angola, Namibia na hata Mauritania, hazikudhaniwa kuwa zitasumbua na kuwa hatari kwenye michuano hiyo.

Pamoja na kwamba zingine kama Mauritania, Namibia hata Gambia zimeondoshwa, lakini unaweza kushangaa zikirudi tena kwenye fainali za mwaka 2025 na kufanya balaa kubwa.

Hii inaonyesha kuwa nchi nyingi zinapotolewa haziendi kulala, bali kuandaa mipango mikakati ya kuhakikisha zinarejea zikiwa na nguvu zaidi kuliko mwanzo.

Kwa nini sasa hivi nchi za Afrika Magharibi siyo tishio kwenye soka peke yake barani Afrika? Ni kwa sababu nchi nyingi sasa hivi zinatoa wachezaji wengi wenye vipaji na wanakwenda kucheza soka la kulipwa nje ya nchi, tofauti na zamani ambao ni nchi hizo timu ndizo zinakuwa nao wengi Ulaya.

Kwa sasa mchezaji yeyote mwenye kipaji, anayejua kusakata soka, hata kama anatoka Tanzania, ni rahisi kupata nafasi kwenda kucheza nje ya nchi tofauti na zamani.

Na hata wanaocheza soka ligi za nyumbani, wanapata bahati ya kukutana na wachezaji wengine wakubwa na hasa wale wanaocheza Ligi ya Mabingwa Afrika au Kombe la Shirikisho, wakikutana hakuna kushangaana wala kuogopana.

Na wala mwaka huu huwezi kushangaa kuona bingwa ikawa ni nchi ambayo haikutegemewa kabisa na inawezekana ikawa ndiyo mara yake ya kwanza kutwaa ubingwa huo.

Kifupi ni kwamba AFCON ya mwaka huu imeonyesha kuwa soka limebadilika kabisa, nchi yoyote inaweza kucheza na yoyote na ikashinda.

Hata hivyo, wakati wachezaji wa Tanzania wakiambia wajifunze hayo, binafsi naona hata waamuzi nao wajifunze kwa wenzake tunaowaona wakichezesha.

Waamuzi hao wanaonekana kupata usaidizi wa VAR kwenye maamuzi makubwa tu, ya bao au siyo bao, lilikuwa la kuotea au sahihi, lakini kwa asilimia kubwa wanachezesha vizuri kwenye maeneo mengi kiasi kwamba kumekuwa hakuna malalamiko makubwa.

Hata hizi timu tunazoziita au kujiita ndogo zimekuwa zikipata ushindi ambao unachagizwa mno na uchezeshaji wa haki wa waamuzi. Tumeshuhudia hata wenyeji Ivory Coast pamoja na kwamba ni uenyeji na kujaza watu viwanjani, lakini imekuwa ikipata tabu sana kwenye matokeo yake kwa sababu hakuna kubebwa.

Waamuzi hawaogopi kuchezesha kwa haki eti kwa sababu wanaichezesha timu yenye mashabiki wengi uwanjani.

Ndiyo maana tulishuhudia ikila mabao 4-0 dhidi ya Equatorial Guinea mbele ya mashabiki wao na maisha yakaendelea, hakuna shabiki aliyemlaumu mwamuzi, badala yake wakawa wanalaumiana wenyewe kwa wenyewe, viongozi, wachezaji, makocha na mashabiki wao.

Kabla hata ya VAR, waamuzi wa Tanzania wanapaswa kuboresha uamuzi wao kwa kuwaangalia wenzao jinsi wanavyofanya hususan kupitia michuano hii ya Afcon ambayo hakuna hata mwamuzi mmoja kutoka nchini alijumuishwa kuchezesha.

Kutokuwapo kwa mwamuzi yeyote kwenye michuano hiyo hakukuja kwa bahati mbaya. Waamuzi wa Tanzania husuan Bara wanafuatiliwa na kukutwa wana makosa mengi, ikiwamo ya kushindwa kutafrisi vema sheria, maslahi, woga na mengine yanayofanana na hayo.

Angalau basi hata AFCON ya 2025 nchini Morocco kabla ile ya 2027 ya Tanzania, Kenya na Uganda, tushuhudie hata mwamuzi mmoja wa Tanzania akipata nafasi ya kwenda kuchezesha, na hili haliwezi kuja kwa upendeleo bali kujirekebisha na kuchezesha kufuata sheria.




Mtaalamu wa Mifumo ya Kompyuta kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Gideon Mwashihongo (katikati), akitoa elimu ya matumizi ya PSSSF Kiganjani App, kwa wanachama wa PSSSF waliotembelea banda la mfuko huo kwenye Maonesho ya Wiki ya Sheria viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam jana. Kupitia PSSSF Kiganjani mwanachama anaweza kupata huduma zote zitolewazo bila ya yeye kulazimika kutembelea ofisi za PSSSF. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkurugenzi, Ofisa Mipango Miji wazomewa mbele ya Makonda

**Na Beatrice Shayo**, KAHAMA

WANANCHI wamemzomea Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama, Anderson Msumba na Ofisa Mipango Miji wa manispaa hiyo, Clemence Mkusa mbele ya Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda.

Ni hali iliyojitokeza juzi wakati wa mkutano wa Makonda alipokuwa anasikiliza kero za wananchi ambao walidai hawawataki watendaji hao.

Wananchi hao waliwatuhumu watendaji hao kwamba wamekuwa chanzo cha migogoro na kupewa majibu waliyoyaita mabovu.

"Makonda ukiondoa Mkuu wa Wilaya anatusikiliza vizuri na Mkuu wa Mkoa anatusikiliza, wanatoa uamuzi lakini mkurugenzi ndiye chachu ya migogoro, anagoma kutusikiliza pamoja na maofisa ardhi lakini kikubwa ni mkurugenzi.

"Mkuu wa Wilaya ameagiza nipimiwe maeneo yangu, lakini mkurugenzi hataki. Anadai kasomea sheria na hafuati mambo ya siasa," alidai Caroline Magige, mkazi wa wilaya hiyo.

Calorine alidai mbele ya Makonda kuwa hawana kiongozi wa kutatua kero zao, akidai mkurugenzi ni chanzo cha migogoro.

"Nimehangaika, leo ni mwaka wa 10 ninahangaika na kesi. Waziri mwezi uliopita katoa maelekezo kuwaambia 'huyu mama siyo mvamizi, ninaomba apatiwe maeneo yake na kama hayapo aelezwe yamekwenda wapi'. Mpaka leo kimya, hakuna utekelezaji," alidai mama huyo.

Kutokana na malalamiko hayo, Makonda alimwita mkurugenzi kuzungumzia jambo hilo huku wananchi wakimzomea.

Naye akatamka kuwa madai ya mwananchi huyo ni ya kisheria.

Hata hivyo, wananchi waliokusanyika kumsikiliza Makonda, hawakutaka kumsikiliza mkurugenzi huyo, wakaendelea kumzomea.

Makonda akataka kujua uzoefu wa mkurugenzi huyo wilayani Kahama, naye akijibu ana miaka minane na awali alikuwa mwanasheria katika wilaya hiyo.

Makonda aliwataka wananchi watulie. Atachukua hatua kuhusu tuhuma hizo walizozitoa.

Awali mama huyo alidai ni mmiliki halali wa kiwanja ambacho kimevamiwa. Tayari wavamizi walishajenga nyumba. Amesharipoti suala hilo kwa viongozi mbalimbali wa serikali bila mafanikio, akiwamo Katibu Tawala wa Wilaya.

Katika mkutano huo, Makonda alibaini karibu kila mwananchi anayesimama, alikuwa na kero ya ardhi, hivyo akaamua kumpigia simu Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Godfrey Pinda na kumtaka kufika katika wilaya hiyo.

"Ninaomba kesho saa mbili watu wote ambao wana kero nje ya migogoro ya ardhi, waje maana tayari nimeshatoa maelekezo kwa Pinda atakuja kushughulikia migogoro ya ardhi na mimi ninabadilisha ratiba yangu, nitakuwapo Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kuhakikisha wananchi wanatatuliwa kero zao," alisema Makonda huku akishangiliwa.

Makonda alimpigia simu Pinda na kumjulisha kumekuwa na migogoro ya ardhi katika wilaya hiyo, hawaridhishwi na maofisa ardhi na kumwomba afike wilayani Kahama.

"Ninachoweza kukuahidi nitakuja hapo kufunga kliniki kubwa ambayo itasikiliza matatizo ya ardhi kwa wananchi hao baada ya Bunge kumakizika, wawe na amani wananchi wangu," alisema Pinda.

Naibu Waziri huyo alisema kwa sasa wanachokifanya wanapitia nidhamu ya utendaji kwa watumishi wao, hivyo atakapofika Wilaya ya Kahama ataanza utekelezaji kufuatilia watumishi wao.

Makonda pia alimtaka Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, kutolea ufafanuzi malalamiko ya huduma mbovu katika Hospitali ya Kahama ikiwamo kulipishwa fedha wanapojifungua.

Mhita alisema kumekuwa na changamoto katika hospitali ya manispaa na wamechukua hatua za kuwasimamisha kazi madaktari na wauguzi waliolalamikiwa.

Alisema hatua ya pili ni kuhakikisha aliyekuwa Mganga Mkuu wa Wilaya na Mganga Mfawidhi wanawapisha katika Wilaya ya Kahama kutokana na changamoto hizo.

Makonda alisema maelezo hayo yanaonesha namna serikali inavyochukua hatua katika matatizo ya wananchi na wasingependa kuona wananchi hawasikilizwi.

Alisema kwa sasa wanachokifanya ni kutaka kupatiwa ripoti ya utendaji kazi wa watumishi ili wananchi wasiendelee kuteseka.

"Tunapokuwa na mkutano ya namna hii inatupa picha kuna watu ambao siyo waadilifu pamoja na mapenzi mema anayoyatoa Rais wetu kwa wananchi wake.

"Huyu mama mjane alivyoeleza, ana haki ya kiwanja chake lakini hapimiwi, anazungushwa hadi mwenyekiti wake wa serikali ya mtaa, wanatafuta kula hela kwake na huyu mwingine ana hati wamekuja watu weupe wamepewa ardhi wakati mmiliki halali yupo," alisema Makonda.

## Bosi mpya wa DART amulika kero wanazolalamikia abiria

**Na Joseph Mwendapole**

MTENDAJI Mkuu wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), Dk. Athumani Kihamia, amewataka watumishi wa wakala huo kufanya kazi kwa weledi, uadilifu, uaminifu na kujituma zaidi ili kuongeza tija katika mradi huo.

Alitoa maelekezo hayo mwishoni mwa wiki alipokutana na watumishi wa wakala kwa lengo la kufahamiana na kuelekezana mikakati ya kuendelea kutoa huduma bora ya usafiri wa umma.

Kikao hicho kilifanyika katika ofisi za wakala zilizoko Ubungo Maji, Dar es Salaam. Hivi karibuni kumekuwa na malalamiko ya utendaji duni katika mradi huo. Uongozi wa juu wa DART umebadilishwa japo haikuelezwa kama mabadiliko hayo yalichangiwa utendaji duni unaolalamikiwa na abiria wanaotumia usafiri wa 'mwendokasi'.

"Tuendelee kutekeleza majukumu yetu kwa weledi, uadilifu na uaminifu muda wote tunapokuwa kazini, pia tuzingatie maadili ya utumishi wa umma hasa suala la kutunza siri za serikali ambalo ni jukumu la kila mmoja wetu, liwe kipaumbele," alisema Dk. Kihamia.

Aliongeza kuwa ni vyema kila mtumishi kufanya kazi kwa mpangilio ikiwa ni pamoja na kuwa na mpangokazi wa siku, wiki na mwezi, jambo ambalo litasaidia kupata mwelekeo wa utekelezaji wa majukumu ya kila mmoja sambamba na kutatua changamoto zinazojitokeza.

"Ninaposema kufanya kazi kwa mpangilio nina maana kuwa na mpangokazi wa siku, wiki na miezi kwa kila mtumishi wa DART kwa kuwa kufanya kazi bila kuwa na dira ambayo ndiyo huo mpangokazi ni sawas na chombo kinachojiendesha bila kuwa na mwelekeo," alisema Dk. Kihamia.

Mtendaji Mkuu huyo pia alisisitiza wakuu wa idara na vitengo kuwa na uelewa wa pamoja katika mipangokazi watakayoandaa ili isitokee kwamba mpangokazi ukawa unajulikana kwa watu wa ngazi za juu pekee bila watumishi wa chini kuufahamu.

Alitolea mfano mpango wa mafunzo kwa watumishi ambao kila mtumishi katika idara anatakiwa kuufahamu ili inapotokea nafasi ya mtumishi kwenda kusoma, isionekane kuwa amependelewa bali ni kwa mujibu wa mpango ambao unafahamika kwa wote.

Dk. Kihamia pia aliwataka watumishi kudumisha upendo na kuepuka tabia za majungu ambazo hazileti tija katika utekelezaji majukumu ya kila siku mahala pa kazi.


Mtendaji Mkuu huyo alitumia kikao hicho kusikiliza changamoto mbalimbali zinazoukabili mradi na namna ya kuzitatua ikiwamo suala la uhaba wa mabasi, kutokuwa na mageti na kadi janja na lugha mbaya na isiyo na staha kwa watumishi.

Changamoto nyingine aliyoelezwa ni pamoja na tatizo la kukatika kwa umeme kunakoathiri utoaji huduma vituoni.

Dk. Kihamia aliteuliwa hivi karibuni na Rais Samia Suluhu Hassan kuchukua nafasi ya aliyekuwa Mtendaji Mkuu wa wakala huo, Dk. Edwin Mhede.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**





Mkurugenzi Mtendaji wa Watumishi Housing Investments (WHI), Dk. Fred Msemwa (kulia), akimkabidhi Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Emmanuel Tutuba, taarifa muhimu za Shirika la WHI walipokutana katika ofisi za BoT Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wizara ya Habari, Benki NMB waingia mkataba kuinua uchumi wa kidijitali

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imetia saini Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) na Benki ya NMB yenye lengo la kuharakisha na kuimarisha ukuzaji wa uchumi wa kidigitali kupitia mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Makubaliano hayo yalitiwa saini na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Mohammed Khamis Abdulla na Ofisa Mtendaji Mkuu, Ruth Zaipuna, wakishuhudiwa na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, hafla iliyofanyika Ijumaa Januari 26, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kutiwa saini makubaliano hayo, Waziri Nape aliishukuru NMB kupitia Mwenyekiti wa Bodi, Ofisa Mtendaji Mkuu, Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na wafanyakazi wa benki hiyo kwa utayari wa kushirikiana na wizara yake kuchochea mabadiliko chanya ya ukuzaji uchumi wa kidigitali.

"Katika kipindi hiki ambacho Tanzania iko kwenye mapinduzi ya nne ya viwanda, tukielekea kwenye mapinduzi ya tano na ya sita, makubaliano haya yanaweka historia na kuthibitisha kuwa TEHAMA na mabadiliko ya kidigitali nchini, ni sekta mtambuka inayogusa sekta ya umma, binafsi na wananchi kwa ujumla.

"Maendeleo ya uchumi wa kidigitali yanapimwa kwa jinsi sekta mbalimbali zinavyotumia TEHAMA kutekeleza majukumu yake na hii inathibitisha kwamba tuko tayari kukimbizana na mabadiliko ya teknolojia katika dunia tunayoiendea na NMB iko tayari kutushika mkono kuyaendea maono hayo," alisema.

Waziri Nape aliongeza: "Dhamira ya serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ni kuona inakuwa na mifumo bora na rafiki ya utoaji huduma kwa wananchi inayotumia teknolojia ya kisasa, pamoja na kuhakikisha tunajenga mazingira wezeshi ya kutumia TEHAMA nchini.

"Pia kuhakikisha tunakuza vipaji vya vijana wetu kwenye masuala ya TEHAMA kwa kuruhusu ubunifu, kuongeza idadi ya vyuo vya ubunifu pamoja na kuongeza ujumuishi wa masuala ya kifedha, ikiwamo kutanua wigo wa matumizi yasiyohusisha fedha taslimu.

"Ndio maana makubaliano haya na NMB tunayapa uzito na thamani kubwa. Kazi yetu kama wizara ni kutengeneza sera, sheria, kanuni, taasisi zitakazozisimamia pamoja na kuweka miundombinu itakayosaidia kujenga huo uchumi wa kidigitali. Ushirikiano huu unakwenda kuongeza kasi ya maendeleo ya TEHAMA," alisema.

Naye Zaipuna alisema makubaliano hayo ni mwendelezo wa uhusiano bora baina ya NMB na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ile ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kujenga uchumi imara wa kidigitali na kwamba anaamini kuwa ni moja ya safari ya kihistoria ya ukuzaji uchumi wa taifa.

"NMB ni mdau mkubwa wa serikali katika kuchagiza Sera ya Uchumi wa Kidigitali, ikiwamo kuunda na kuboresha mifumo ya TEHAMA, ambapo hivi karibuni tulitia saini makubaliao na Mamlaka Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) kutengeneza mfumo wa usajili na kutoa vibali kwa wawekezaji.

"Pia tumetia saini makubaliano na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, ili kutengeneza mfumo wa kuomba vibali vya watalii na kufanya malipo, kama tulivyotia saini pia na Wizara ya Mambo ya Nje kutengeneza kanzidata ya watanzania wanaoishi nje yaani Diaspora.

"Hiyo ni mifano michache tu ya maeneo ambayo tayari NMB imeshirikiana na serikali zote mbili. Makubaliano haya yatashuhudia NMB ikishirikiana na wizara kuchagiza uchumi wa kidigitali na baadhi ya maeneo ya kimkakati yatakayoguswa ni kutengeneza mifumo ya kidigitali ikiwa pamoja na Jamii Namba (utambuzi wa mwananchi kurahisisha utoaji huduma kimtandao).

"Maeneo mengine ni kutengeneza mfumo wa 'Jamii Data Exchange' utakaosaidia kuunganisha mifumo ya serikali katika sehemu moja, ili kuziwezesha kupata taarifa zote kwenye mfumo mmoja na uundwaji mifumo imara zaidi ya malipo mitandaoni kwa lengo la kuwezesha huduma salama na rahisi za miamala ya kidigitali.

"Pia tutasaidia wabunifu na wajasiriamali hasa wa sekta ya fedha kupitia vyuo vya ubunifu vitakavyoanzishwa na wizara yako na pia tutatumia wataalamu wetu kuunda na kuboresha mifumo tuliyoitaja na kutoa jukwaa la kufanyia majaribio ya mifumo, tukiamini katika uwekezaji tuliofanya kwenye eneo hilo," alisema.

Awali akimkaribisha Waziri Nape, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Mohamed Khamis Abbdulla, alisema kilichofanywa na pande mbili zilizotia saini makubaliano hayo ni kuunga mkono juhudi za Rais Samia ambaye amedhihirisha dhamira ya dhati ya kuliendeleza taifa kupitia uchumi wa kidigitali kwa kuunda wizara hiyo mnamo Septemba 12, 2021.

"Aliunda wizara hii na kuipa jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera ya TEHAMA na kwa nyakati tofauti imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali kutekeleza masuala tofauti, kama tunavyoshuhudia leo ikitia saini makubaliano na NMB kuharakisha ukuaji uchumi wa kidigitali.

"Tukio hili ni mwendelezo wa ushirikiano ambao wizara yako tumefanya hivi si tu na taasisi za ndani, bali pia za kimataifa ili kuongeza ushindani na NMB wamekuwa wadau muhimu walioshirikiana nasi katika maeneo mengi sana ikiwamo uandaaji Mpango Mkakati wa Miaka 10 ya Uchumi wa Kidigitali na uandaaji wa Sera Mpya ya TEHAMA ya 2024," alifafanua.

# Wajasiriamali, walimu 700 wapatiwa mitungi ya gesi na majiko

**Na Gwamaka Alipipi**

WALIMU na wajasiriamali zaidi ya 700 wilayani Kisarawe, mkoani Pwani wamekabidhiwa mitungi ya gesi na majiko kwa lengo la kuwawezesha kutumia nishati safi ya kupikia ili waachane na matumizi ya kuni na mkaa.

Msaada huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Waziri wa Nchi Ofisi ya Mwakamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo aliyeshirikiana na kampuni ya Oryx Gas Tanzania.

Katika hafla ya kukabidhi vifaa hivyo kwa walimu wa shule za msingi na sekondari zaidi ya 500, Mkurugenzi wa Kampuni ya Oryx Gas Tanzania, Benoit Araman, alimshukuru Dk. Jafo kwa kumpatia nafasi ya kupeleka nishati safi ya kupikia kwa walimu pamoja na babalishe na mamalishe wilayani Kisarawe.

"Oryx Gas tunaamini kwamba ukipika kwa kutumia gesi, inaleta maendeleo mengi kwa jamii yetu, pia inalinda mazingira kwa kuacha kukata miti.

"Zaidi ya yote ni kulinda afya ya wanawake kwa kuwaepusha kuvuta moshi na mvuke unaoathiri mapafu na afya yao unaotokana na kuni na mkaa," alisema.

Alibainisha kuwa kuanzia Julai 2021, wamekuwa mstari wa mbele kutekeleza maelekezo ya serikali waliyopokea kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan kwamba ifikapo mwaka 2032, asilimia 80 ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia.

Araman alisema mkakati wao ni kutokomeza matumizi ya nishati ya kuni na mkaa.

Alisema Oryx Gas inatekeleza agizo la serikali kwa kuhakikisha taasisi zenye watu zaidi ya 100 zinatumia nishati safi kwa kutengeneza mifumo salama ya gesi kwa kutumia tangi kubwa ambapo mifumo hiyo inaweza tumika shuleni, kambi za jeshi, vyuo vya polisi na magereza.

Hivyo, aliwahimiza wananchi kutumia gesi ya LPG katika shughuli zao ili kuleta maendeleo nchini pamoja kuboresha maisha.

Vilevile, alisema wana mkakati wa kufunga mfumo wa nishati safi ya kupikia katika Shule ya Sekondari Minaki iliyoko wilayani Kisarawe.

Alisema watafunga mfumo huo ili shule hiyo iondokane na matumizi ya kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia.

Alisema watafunga mfumo wenye uwezo wa kubeba ujazo wa tani moja ya gesi.

Waziri Jafo aliishukuru kampuni hiyo kwa kuendelea kuunga mkono juhudi za Rais Samia katika kuhamasisha matumizi ya nishati safi kwa vitendo.

Alisema tayari serikali imeshatoa maelekezo kuanzia mwaka huu taasisi, mashirika na maeneo ambayo yana watu kuanzia 100 kuanza kutumia nishati safi ya kupikia ikiwamo gesi.

Waziri huyo alisema mbali na kutolewa msaada huo, ataendelea kuzungumza na wadau ili apate mitungi mingine, lengo lake ni kuhakikisha walimu wote 1,300 wilayani Kisarawe wanatumia gesi kwa matumizi yao ya nyumbani.

# Wajumbe waridhishwa utekelezaji miradi

Na Allan Isack, ARUSHA

WAJUMBE wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kata ya Themi, Wilaya ya Arusha, mkoani hapa wameonyesha kuridhishwa na utekelezaji wa ilani ya chama hicho kwa kipindi cha miezi sita mwaka jana.

Kabla ya kuanza kwa kikao cha Halmashauri Kuu, Kamati ya Siasa ya Kata ya Themi, wajumbe hao walifanya ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi kwa kipindi hicho kuanzia Julai hadi Desemba mwaka 2023.

Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa katika Shule ya Msingi ya Arusha, kivuko cha watembea kwa miguu kinachounganisha na kata hiyo ya Themi na Kati na ujenzi wa jengo la mama na mtoto lililopo Kituo cha Afya cha Themi.

Akisoma taarifa ya utekelezaji wa Ilani hiyo kwa kipindi hicho mbele ya wajumbe hao, Diwani wa Kata ya Themi, Lobora Ndarpoi, aliishukuru serikali kwa kutoa fedha za utekelezaji wa miradi hiyo katika kata hiyo.

Diwani Ndarpoi, alisema serikali imetoa Shilingi milioni 60 kwa ajili ya ujenzi wa mdarasa hayo na kukamilika kwa zaidi ya asilimia 98.

Alisema serikali pia imetoa Shilingi milioni 200 kwa ujenzi wa jengo hilo katika kituo hicho cha afya kwa lengo la kuboresha huduma za afya kwa mama na mtoto, hivyo kumaliza kilio cha wakazi wa kata hiyo cha muda mrefu.

Kwa mujibu wa diwani huyo, serikali imetoa kiasi kingine cha Shilingi milioni 14.76 kujenga kivuko cha watembea kwa miguu kinachounganisha kata hizo na kuwasaidia wanafunzi kukabiliana na changamoto ya aina yoyote.

"Katika kwa kipindi hicho, tumejenga barabara kwa kiwango cha lami na nyingine kuweka changarawe hasa maeneo korofi ili kuhakikisha zinapitika wakati wote," alisema na kuongeza kuwa:

"Naishukuru Serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuipatia kata yetu fedha nyingi za kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kuwa itakuwa chachu kuleta maendeleo kwa kasi na kukuza uchumi na kipato kwa mwananchi mmoja mmoja."

Katibu wa CCM wa Kata hiyo, Deus Kitinde, ambaye ni mwenyekiti wa kikao hicho, alimpongeza Ndarpoi kwa kusimamia na kutekeleza ilani ya chama hicho.

Alisema CCM kitaendelea kutoa ushirikiano kwa diwani huyo na watendaji wote wa serikali ili kuhakikisha inatimiza dhamira ya kupeleka maendeleo kwa wananchi.

Katibu wa Siasa na Uenezi CCM wa Themi, Catherine Nyabamba, alisema chama hicho kitaendelea kuisimamia serikali ili kuhakikisha ilani hiyo inatekelezwa kama walivyoahidi kwa wananchi.




Mkurugenzi wa Kampuni ya Oryx Gas Tanzania, Benoit Araman (wa tatu kushoto), akimkabidhi mtungi wa gesi ya Oryx Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Dk.Seleman Jafo, ikiwa ni sehemu ya mitungi 700 iliyotolewa na kampuni hiyo kwa ajili ya kuigawa kwa walimu 500 pamoja kwa baba na mamalishe 200 Wilaya ya Kisarawe, mkoani Pwani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Polisi yawakumbusha wazazi wajibu

Na Allan Isack, MONDULI

JESHI la Polisi limewahimiza wakazi wa Kijiji cha Lengelorti Kata ya Naalarami wilayani hapa Mkoa wa Arusha kuwatimizia mahitaji watoto wao kwa kuwanunulia sare na vifaa vya kusomea ili kuhakikisha wanapata elimu bora na kudhibiti utoro.

Rai hiyo imetolewa jana na Mkaguzi Msaidizi wa Polisi wa Kata hiyo, Musa Stephen, wakati wa kikao baina ya maofisa wa jeshi hilo na wakazi hao kilichofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita kijijini hapo.

Stephen alisema ni wajibu wao kuwanunulia watoto wa sare za shule, vifaa vya kusomea na kuwapa chakula cha mchana wanapokuwa shuleni.

"Wazazi mnatakiwa kutimiza wajibu wenu na haki za watoto ikiwa ni pamoja na kuhakikisha mnawalea vema na kuwapatia matibabu wanapougua," alisema Stephen.

Naye Mkaguzi Msaidizi wa Polisi Kata ya Moita Bwawani, Mathew Michael, aliwaasa wafanyabiashara kuacha tabia ya kuhifadhi mafuta ya petroli kwenye maduka ya vyakula.

Akizungumza na baadhi ya wafanyabiashara katika kata hiyo, alionya kuwavitendo hivyo vinaweza kusababisha ajali ya moto na kuleta madhara katika jamii. "Kutokuwa na vituo vya kuuzia mafuta ya petroli au dizeli kijijini hapa isiwe tiketi ya nyie kuhifadhi mafuta ya aina hii kwenye makazi yenu kwa nia ya kufanya biashara.

"Kila kitu kina utaratibu uliowekwa na serikali kupitia mamlaka zake na ndio unasababisha tuwe katika mazingira salama," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya wafanyabiashara wa kijiji hicho, Piniel Lukumay maarufu kwa jina la Lemali, ameshukuru kwa elimu hiyo iliyotolewa na Polisi na alisema wameipokea kwa mikono miwili na kuahidi kuifanyia kazi kwa manufaa yao na jamii.

## RC Mongela aipongeza mahakama

Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA

MKUU wa Mkoa Arusha, John Mongella, ameipongeza idara ya mahakama jijini hapa kwa kumaliza kero ya kuchelewesha kutoa nakala za hukumu kwa wakati na malalamiko ya wananchi.

Mongella alitoa pongezi hizo mwishoni mwa wiki iliyopita jijini Arusha kwenye Maadhimisho ya Wiki ya Sheria kwa mwaka huu yanayoendelea nchini.

Alisema maadhimisho hayo yamenufaisha wananchi wengi kwa kupata elimu na msaada wa kisheria bure.

"Nawapongeza sana mfumo wa Mahakama umeimarika, hatupati tena malalamiko ya kuchelewa kupokea nakala za hukumu kama ilivyokua huko nyuma, hii ni hali halisi inayoonyesha utendaji kazi wa mhimili huu umeboreshwa sana kupitia mifumo ya TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano)," alisema.

Alisema mrundikano wa kesi zisizosikilizwa unazidi kupungua na kuleta matumaini kwa wananchi na wadau wa mahakama nchini kutokana na matumizi ya TEHAMA.

Mongela alisisitiza kuwa mfumo wa utoaji haki ukiimarika zaidi, kesi zikiisha kwa wakati na misaada ya sharia ikitolewa mara kwa mara, kutawapunguzia wananchi kutumia muda mwingi kuhangaika na mashauri mahakamani na badala yake kushiriki katika maendeleo. Jaji Mafawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Arusha, Joachim Tiganga, alisema kuanzia Januari 24 wamekuwa na utoaji wa elimu shuleni, vyuoni na maeneo mengine ya jamii kama ishara ya uzinduzi wa wiki hiyo nchini.

"Wiki hii tumeianza Januari 24 hadi 30 kwa kutoa elimu ya kisheria bure kwa wananchi hi kilele chake Februari Mosi mwaka huu, pia tutakuwa na bonanza kwa wadau wa mahakama ili kujenga mshikamano zaidi na kuimarisha mwili.

Alisema kauli mbiu ya mwaka huu

"Umuhimu wa dhana ya haki kwa ustawi wa taifa. Nafasi ya Mahakama na wadau katika kuboresha mifumo jumuishi wa Haki Jinai" inamezingatia mahitaji ya Taifa na jamii.

Jaji Tiganga, alisema kauli mbiu hiyo watatembea nayo mwaka mzima na kila mwaka wanakuwa na kauli mbiu inayowaongoza katika utendaji kazi wao kwa mwaka mzima.

Naibu Msajili wa Mahakama Kuu Kanda Arusha, Mariam Mchomba, alisema katika wiki hiyo wametoa elimu kwa makundi hayo na kufanya shughuli mbalimbali ikiwa ni ishara ya kuanza kazi za mahakama.





# Wasichana waliokatisha masomo wapata mfadhili

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

ZAIDI ya wasichana 170 waliocha shule baada ya kupata ujauzito na ndoa za utotoni katika Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga wamepata ufadhili wa mafunzo katika Chuo cha Ufundi Msaginya (FDC) kilichopo wilayani Mpanda Mkoa wa Katavi.

Wasichana hao wamepata ufadhili huo kutoka Taasisi ya Msalala Foundation iliyopo chini ya Mbunge wa Msalala, Iddi Kassimu ili kuhakikisha wanatimiza ndoto zao kuajiriwa na kujiajiri baada ya kuhitimu mafunzo yao.

Katibu wa Mbunge huyo, Edson Erasto, aliyabainisha hayo jana wakati akiwakabidhi wasichana wengine 60 waliochaguliwa kujiunga masomo kwa mwaka huu wa 2024 kwa Mkuu wa chuo hicho, Leonard Mwambije.

Alisema ofisi ya mbunge huyo, imekuwa mstari wa mbele kusaidia wasichana na vijana wanaotoka katika mazingira magumu wafikie malengo yao.

Alisema wasichana hao, wanafanya idadi yao kufikia 170 ya waliofadhiliwa na Msalala Foundation kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo.

Kwa mujibu wa Erasto, mwaka 2022 taasisi hiyo ilifadhili wasichana 60, mwaka jana 50 na mwaka huu 60 kutoka kata 18 za Halmashauri ya Wilaya ya Msalala.

Alisema wasichana hao walipatikana kupitia kwa maofisa watendaji wa kata husika, walimu wakuu wa shule za msingi na sekondari walikokuwa wakisoma kabla ya kukatisha masomo.

Kwa upande wake, Mwambije alipongeza taasisi hiyo kwa kurejesha matumaini kwa wasichana hao ya kujiajiri au kuajiriwa baada ya kupata elimu ya ufundi.

Mmoja wa wasichana hao, Jasmin Godfrey, alisema alishinwa kutimiza ndoto yake ya kuwa daktari baada ya kukatisha masomo na kuwataka wanafunzi wa kike kuepuka vishawishi na tamaa ili wamalize masomo.

Alisema ufadhili huo umeamsha matumaini yake ya kujiajiri na kuajiriwa baada ya kuhitimu ufundi katika chuo hicho.



Mkuu wa Wilaya ya Sikonge, mkoani Tabora, Simon Chacha (kushoto), akipokea zawadi ya kitabu kutoka kwa Mhamasishaji Ofisi ya Shirika la Akili Platform Tanzania (APT), upande wa wenye mahitaji maalum, Deborah Daniel, alipotembelea banda la APT katika maadhimisho ya Wiki ya Sheria, mjini Tabora mwishoni mwa wiki. Katikati ni Mkurugenzi Mtendaji APT, Roghat Robert. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madiwani walalamikia vituo mafuta kukusanya mapato

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MADIWANI wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga wamelalamikia mapato ya maegesho ya magari ya mizigo kukusanywa na baadhi ya wamiliki wa vituo vya mafuta na kuongeza mianya ya upotevu wa fedha kwa ajili ya maendeleo.

Malalamiko hayo yaliibuka juzi katika kikao cha robo tatu ya mwaka wa baraza la madiwani hao.

Madiwani hao walisema kuwa wana eneo la maegesho la magari hayo walilopewa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADs), lakini yamekuwa yakiegeshwa kwenye vituo vya mafuta na maeneo ya wazi na kuikosesha manispaa hiyo mapato.

Diwani wa Viti Maalum, Herieth Makaga, alisema ukusanyaji wa mapato yatokanayo na maegesho ya magari wameachiwa baadhi ya wamiliki wa vituo hivyo na kutoa mianya ya upotevu wa fedha za manispaa yao.

Akizungumzia malalamiko hayo, Kaimu Mweka Hazina wa Halmashauri hiyo, Neema Kabuje, alisema wamewekа vituo vya mafuta kuwa mawakala wa ukusanyaji wa mapato hayo ya maegesho hayo.

Mjumbe wa Kamati ya Uchumi Mipango na Fedha wa Manispaa hiyo, Vaileth Bulili, alisema hawajawahi kujadili wala kupitisha hoja ya vituo vya mafuta kukusanya mapato hayo. Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Robert Kwela, alisema eneo linalomilikiwa na manispaa yao ni dogo na limezidiwa na magari hayo na kulazimu kuegeshwa kwenye vituo hivyo na maeneo ya wazi

Kwela, alisema wanafanya uchunguzi kubaini magari hayo yanayoingia katika mji wa Kahama na kwamba wanatarajia kuweka mfumo wa kidigitali ili kudhibiti upotevu wa mapato ya maegesho katika maeneo ya wazi na vituo hivyo vya mafuta.

# Washauriwa kufuata suluhu ya migogoro mahakamani

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

JAMII imetakiwa kutumia Mahakama kusuluhisha migogoro badala ya njia ya mkato ya kumalizana kwa kukubali yaishe kwa kuwa kunachochea uhasama katika jamii.

Wito huo ulitolewa juzi na Hakimu Mfawidhi wa Wilaya ya Sengerema, Tumsifu Barnabas wakati wa ufunguzi Wiki la Sheria.

Hakimu Barnabas, alisema wananchi wakiwamo wakazi wa wilayani hapa wanapaswa kuacha kuogopa mahakama kwa sababu ni chombo ambacho kinatoa haki kwa njia sahihi. Alisema utaratibu wa kumalizana wao kwa wao umekuwa ukisababisha kukua kwa migogoro na wakati mwingine kujichukulia sheria mkononi baada ya kukandamizwa.

Alisema kuwasilisha migogoro yao mahakamani ni sehemu pekee ambako haki stahiki inapatikana. Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Ngaga, akizungumza katika maadhimisho hayo, aliwataka watumishi wa mahakama kuhakikisha wanatekeleza wajibu wao ipasavyo na kuondoa malalamiko ya mara kwa mara.

Ngaga, alitumia fursa hiyo kuwaagiza wazazi kuwapeleka watoto wao shule wenye umri wa kuanza darasa la kwanza na waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu.

Alionya kuwa serikali haitawafumbia macho wazazi watakaokiuka agizo hilo kwa sababu lipo kwa mujibu wa sheria.

Mkuu wa Mashtaka Wilaya ya Sengerema, Dorikas Akio, alisema wananchi wanatakiwa kutoa taarifa za kucheleweshwa kwa mashtaka na ukiukwaji wa sheria ili kupata ufafanuzi.

Ofisa Uhamiaji wa Wilaya ya Sengerema, Titus Mrefu, aliwataka wananchi kuwafichua raia wa kigeni wanaoishi kwenye maeneo yao na kufanya kazi bila kibali ili wachukuliwe hatua.

Maadhimisho hayo ya Wiki ya Sheria kwa Sengerema, yanafanyika katika Kijiji cha Busisi Kata ya Busisi.

Nipashe
Spotika



TULICHOJIFUNZA AFCON HATUAYA MAKUNDI UK. 12



# WACHEZAJI 9 WANAOVUTIA ZAIDI AFCON

Achraf Hakimi

**ABIDJAN, Ivory Coast**

MICHUANO ya kombe la Mataifa ya Afrika, Afcon, hivi sasa ipo hatua ya mtoano wa timu 16 bora, baada ya mambo mengi ya kuvutia kwenye hatua ya makundi. Na kuna nyota ambao wamejitosa na kujitangaza zaidi katika mashindano haya kwa viwango vyao bora vya uchezaji.

Makala haya yanawaangalia wachezaji ambao hadi sasa wamevutia machoni kwa watazamani wengi wa michuano hiyo.

**Emilio Nsue Lopez (Equatorial Guinea)**

Nahodha wa Equatorial Guinea, ameibuka kinara katika hatua ya makundi, akifunga mabao matano katika mechi tatu tayari. Licha ya kuwa ni mlinzi wa klabu yake ya CF Intercity ya nchini Hispania, mchezaji huyo wa zamani wa Middlesbrough na Birmingham City anaongoza safu ya ushambuliaji katika timu yake ya taifa. Akiwa na mabao matatu ya ajabu dhidi ya Guinea Bissau na mabao mawili dhidi ya wenyeji Ivory Coast, Nsue ni mshindani mkubwa wa tuzo ya kiatu cha dhahabu.

**Georges-Kevin N'koudou (Cameroon)**

Akiwa na msaada wa kufunga mabao mara tatu kwenye michuano hiyo, winga wa Cameroon, Nkoudou ni mmoja wa waliobadilisha mchezo kwenye Afcon. Huenda Simba Wasiofugika walitatizika kupita hatua ya makundi, lakini kiungo huyo anayecheza Saudia hajashindwa kufanya vizuri wakati muhimu zaidi. Misaada yake mara mbili katika mchezo wa mwisho wa kundi dhidi ya Gambia, uliokoa ushindi wa mabao 3-2 kwa Simba hao, ambao jana walicheza na Nigeria katika hatua ya 16 bora.

**Sadio Mane (Senegal)**

Wengi walidhani kwamba uhamisho wa fedha nyingi wa Sadio Mane kwenda Klabu ya Saudi Aarabia, Al-Nassr ungeweza kuashiria mdororo wa mchezo kwa winga huyo wa Senegal, lakini mwanasoka huyo bora wa mwaka wa Afrika mara mbili anadhihirisha kwa wenye shaka kuwa sio sahihi nchini Ivory Coast. Akija kwenye dimba hilo, siku chache baada ya harusi yake, Mane amekuwa na ushawishi mkubwa katika uchezaji wake kwa mabingwa hao watetezi kwenye hatua ya makundi, akiwa na bao moja na asisti mbili.

**Achraf Hakimi (Morocco)**

Hakimi amekuwa moyo wa Simba wa Atlas (Morocco) kwenye Afcon hadi sasa. Akiwa na bao pamoja na asisti kwa jina lake, Hakimi amehusika kwenye mabao mengi yaliyofungwa kwa kikosi hicho, akitengeneza tishio kubwa kutoka kwenye winga na mipira ya adhabu ndogo.

**Gelson Dala (Angola)**

Gelson Dala alifunga mabao mawili wakati Angola ilipoilaza Mauritania 3-2 katika moja ya mchezo wa kuburudisha sana wa Afcon hii. Mchezaji huyo wa Angola amekuwa mzuri kwa kuiongoza nchi yake katika michuano hiyo kwa kasi yake ya kulipuka na ustadi wa kucheza chenga na kusababisha matatizo kwa wapinzani. Mshambuliahi huyo anayecheza nchini Qatar, anatarajiwa kuimarika katika kiwango chake kizuri kwa 'Palancas Negras. hao katika hatua hii ya mtoano.

**Stanley Nwabali (Nigeria)**

Kuingia kwa Afcon mwaka huu, wasiwasi mkubwa wa Nigeria ulikuwa kuhusiana na nafasi ya golikipa huku mashabiki wakihoji uwezo wa makipa, Francis Uzoho na Maduka Okoye. Mchezaji wa Chippa United, Stanley Nwabali aliingia pichani kwa ajili ya Nigeria usiku wa kuamkia mchuano huo na alicheza mechi yake ya kwanza tu wakipoteza kwa mabao 2-0 katika mchezo wa kirafiki wa awali dhidi ya Guinea. Onyesho lake la hadi sasa kwenye dimba, limekuwa msaada mkubwa kwa safu ya ulinzi ya Super Eagles hao.

**Lamine Camara (Senegal)**

Mwanasoka huyo bora chipukizi wa Afrika amejitangaza kwenye onyesho kubwa zaidi la soka barani Afrika kwa kufunga mabao mawili na kufanya vema kwa mabingwa hao watetezi katika mechi yao ya ufunguzi dhidi ya Gambia. Baada ya kushinda Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Vijana wenye umri wa chini ya miaka 20 na Ubingwa wa Mataifa ya Afrika (Chan), Camara anaweza kuwa kito cha thamani kwa dimba hilo huku klabu za Ligi Kuu England vikimmezea mate kinda huyo mwenye umri wa miaka 20.

**Mohammed Kudus (Ghana)**


Huenda ikawa kampeni ya kutamausha kwa Black Stars ya Ghana kwenye Afcon, lakini Mohammed Kudus wa West Ham, aliridhisha matarajio ya wengi licha ya kusumbuliwa na majeraha. Alikosa kichapo cha 2-1 dhidi ya Cape Verde katika mechi ya kwanza ya kundi la Ghana, lakini akarejea kwa kufunga mabao mawili katika mchezo bora dhidi ya timu ya Mo Salah ya Misri. Alipata tena tuzo ya mchezaji bora wa mechi katika sare ya 2-2 dhidi ya Msumbiji katika mchezo wao wa mwisho wa kundi, ambao ulihitimisha matumaini ya Ghana kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

**Aboubakary Koita (Mauritania)**

Bila shaka Mauritania ni moja ya timu za kushtukiza kwenye Afcon na mtu mmoja, anayeendesha ndoto ya timu kwenye mashindano hayo ni Aboubakary Koita. Miondoko yake ya kasi, uchezaji wa winga na jicho la kulenga lango kumeisaidia nchi yake kutinga hatua ya 16 bora, waliyoipata kwa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya mabingwa wa Afcon 2019, Algeria. Bila shaka Koita ndiye wa kuangaliwa katika hatua inayofuata ya shindano hilo.

## ISIKUPITE

HAT-TRICK aliyofunga mshambuliaji wa Equatorial Guinea, Emilio Nsue mwenye miaka 34, wakati wakiichapa Ivory Coast 4-0 kwenye hatua ya makundi Afcon, ni ya kwanza kufungwa baada ya miaka 16 katika michuano hiyo, pia inamfanya kuwa mchezaji wa 17 kufunga hat-trick kwenye mashindano hayo tangu yalipochezwa kwa mara ya kwanza nchini Sudan 1957. Lakini pia hiyo inakuwa hat-trick ya 18 tangu michuano hiyo ianzishwe



## Extra Time

# TULICHOJIFUNZA AFCON HATUA YA MAKUNDI


Emilio Nsue akipongezwa na wachezaji wenzake wa Equatorial Guinea baada ya kufunga hat-trick dhidi ya Ivory Coast kwenye hatua ya makundi ya michuano ya Afcon inayoendelea nchini Ivory Coast.

**ABIDJAN, Ivory Coast**

MSHTUKO mkubwa, ushujaa wa dakika za mwisho, wingi wa mabao na hitilafu nyingi ambazo waandishi wa 'scripti' za muvi za Hollywood wanaweza kudhani kuwa ni za kustaajabisha sana - hatua ya makundi ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), ilionekana kuwa kila kitu.

Wenyeji Ivory Coast walikaribia kushindwa, timu ambazo hazikuwa na shauku zilishinda kwa raha katika makundi yao na wachezaji mashuhuri walifunikwa kwa kiasi kikubwa na majina yasiyojulikana sana ambao walionekana kudhamiria kuweka mshangao.

Kisha kulikuwa na awamu ya kuepukika ya kuondoka kwa makocha wa timu kabla ya kuelekea kwenye fainali.

Mashabiki wa kandanda wako katika tafrija kwenye hatua ya mtoano iliyoanza Jumamosi kama itaendelea na kasi hiyo. Wakati huo huo, BBC Sport Africa inaangalia nyuma kwenye ufunguzi usiotabirika wa siku 11 katika njia ya kuamua nani atakuwa bingwa wa bara la Afrika.

### Wakubwa wachechemea, wadogo wang'ara

Nigeria wakitoka nyuma na kupata pointi moja dhidi ya Equatorial Guinea katika mechi ya pili pekee ya michuano hiyo, walidokeza tu misukosuko ijayo.

Rekodi ya mabingwa mara saba Misri walichukua nafasi ya mbele baada ya sekunde 89 dhidi ya Msumbiji, lakini walihitaji penalti ya dakika ya 97 kutoka kwa Mohamed Salah ili kupata sare ya 2-2, na hivyo kuweka sauti ya furaha ijayo.

Washindi wa zamani Ghana, Algeria na Tunisia wote walishindwa kutinga hatua ya 16 bora, huku Equatorial Guinea, Cape Verde na Angola zote zikimaliza zikiwa juu katika makundi yao.

Ivory Coast ilipokea kichapo cha kushangaza cha mabao 4-0 kutoka kwa Equatorial Guinea katika mechi yao ya mwisho ya Kundi A, ikitazamwa na mshambuliaji wao mashuhuri na mshindi mara mbili wa fainali hizo, Didier Drogba.

Wenyeji hao wa Afrika Magharibi walifikia rekodi yao isiyo na mvuto ya kuwa taifa pekee mwenyeji kupoteza michezo miwili ya makundi, wakiwa wa kwanza kufanya hivyo walipoingia kwenye michuano hiyo mwaka 1984.

Bila shaka mshtuko wa hatua ya makundi ulikuja kwa hisani ya Namibia, huku timu hiyo iliyoorodheshwa katika nafasi ya 115 kwa ubora duniani ikipata ushindi wake wa kwanza kwenye michuano hiyo kwa kuwalaza mabingwa wa mwaka 2004 Tunisia bao 1-0.

Ushindi huo uliwasaidia kusonga mbele, huku kukiwa na nyakati zisizoweza kusahaulika.

Katika usiku uleule ambao Mauritania iliishinda Algeria na kuwalaza mabingwa hao wa mwaka 2019, Gambia na Cameroon zilishiriki katika mchezo wa ajabu wa Kundi C.

'Simba Wasiofugika' (Cameroon) ambao ni washindi mara tano wa Afcon, walikuwa kwenye wakati mgumu katika michuano hiyo walipopata bao la kuongoza dakika ya 85, lakini mabao mawili ya dakika za mwisho yaliwafanya Waafrika ya Kati hao wasonge mbele.

Mabingwa watetezi Senegal, kwa upande wao, walitinga hatua ya 16 bora wakiwa timu pekee yenye rekodi ya ushindi kwa asilimia 100.

### Usipepese macho hatua za kufunga

Mostafa Mohamed alifunga bao alilofikiri ni la ushindi dakika ya 93 dhidi ya Cape Verde, lakini bado kulikuwa na mchezo wa kuigiza mbele yake.

Kumekuwa na mabao 12 katika muda wa majeruhi wa kipindi cha pili kwenye fainali hizo- mara nne ya idadi ya ile ya mwaka 2021 nchini Cameroon - na takriban yote yakiwa yasiyotarajiwa kabisa.

Garry Rodrigues alitumia vema nafasi yake na kuipa Cape Verde ushindi wa dakika ya 92 dhidi ya Ghana na kuwaweka Black Stars kwenye presha.

Ghana walirejea uwanjani na walikuwa tayari kupita Kundi B kabla ya uongozi wao wa mabao 2-0 kusawazishwa dakika za 91 na 94 na Msumbiji na kutolewa hatua ya makundi.

Pia kulikuwa na kuchelewa katika mchezo wa mwisho wa Misri, kwani Waafrika Kaskazini hao walitangulia mbele katika dakika ya 93 dhidi ya Cape Verde, lakini wakakubali bao la kusawazisha dakika ya 99.

Hata hivyo, Mafarao walifanikiwa kupenya mbele ya Ghana licha ya kutoka sare katika michezo yote mitatu ya kundi.

Kwingineko, Burkina Faso walisonga mbele nyuma ya mkwaju wa penalti wa Bertrand Traore dakika ya 96 dhidi ya Mauritania, lakini bao la kichwa la Baghdad Bounedjah dakika ya 95 ambalo liliipa sare dhidi ya Burkinabe halikuweza kuwasaidia Algeria.

Kulikuwa na mabao matatu kati ya dakika ya 86 na 90 katika mechi mbili zilizopita, lakini wakati huu kumekuwa na tano.

Bao la ushindi la Deon Hotto kwa Namibia dhidi ya Tunisia lilipatikana zikiwa zimesalia dakika mbili kabla ya mechi kumalizika na Cameroon wakajicharaza kurejea dimbani dhidi ya Gambia kupitia kwa James Gomez aliyejifunga dakika ya 87 kabla ya Christopher Wooh kufunga bao la ushindi kwa Simba wasiofugika hao dakika moja baada ya muda wa nyongeza.

Mabao hayo yamesaidia michuano hiyo kufikisha wastani wa mabao 2.47 kwa kila mchezo, ingawa pengine ni matumaini kutarajia kiwango hicho kuendelea wakati huu wa mtoano.

### Salah, Kudus wateseka, Osimhen ajitafuta

Mohamed Salah ndiye mchezaji mwenye hadhi ya juu zaidi katika michuano hii ya Afcon, na umakini wa fowadi huyo wa Liverpool umeongezeka kabla ya kulazimika kutoka nje kipindi cha kwanza katika sare ya 2-2 ya Misri dhidi ya Ghana kutokana na jeraha la misuli ya paja.

Baada ya kushika nafasi ya pili kwenye fainali za 2017 na 2021, Salah amezungumzia dhamira yake ya kutwaa taji hilo kwa mara ya kwanza, lakini amerejea Anfield kwa matibabu ya tatizo ambalo linaonekana kutomruhusu kurejea kwenye michuano hiyo.

Mchezaji wa West Ham, Mohammed Kudus aliendelea na kiwango chake cha kuvutia cha klabu kwa kufunga mabao yote mawili ya Ghana dhidi ya Misri katika mchezo huo, na kuachwa akionekana kuhuzunika baada ya nchi yake kucheza na Msumbiji, ambapo aliilaumu kwa kupoteza umakini.

Mwanasoka Bora wa Mwaka wa Afrika aliyetawazwa hivi karibuni, Victor Osimhen bado hajaweza kurejea katika kiwango kizuri alichopata alipofunga mabao mengi zaidi kwenye Serie A msimu uliopita na kuiwezesha Napoli kutwaa ubingwa.

Osimhen, hata hivyo, ana takwimu za juu zaidi za mabao yanayotarajiwa na majaribio ya kulenga lango kwenye fainali za Afcon, baada ya kupiga mashuti 13.

Nyota hao wote wamezidiwa na mshambuliaji Emilio Nsue mwenye umri wa miaka 34 wa Equatorial Guinea, ambaye aliwahi kuichezea Middlesbrough na Birmingham City na ndiye mfungaji bora wa michuano hiyo hadi sasa akiwa na mabao matano.

Mfungaji wa hat-trick ya kwanza ya Afcon ndani ya miaka 16 na mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi kuwahi kufunga 'hat-trick' kwenye michuano hiyo, Nsue alifunga mabao mawili dhidi ya Ivory Coast yaliisaidia timu yake kuongoza kundi A kwa kushangaza.

### Makocha kutimuliwa, kusimamishwa

Wakati majina makubwa yanapotoka kwenye mashindano, makocha hulipa gharama yake.

Ghana ilimfukuza kazi mara moja Chris Hughton baada ya kuondolewa kwenye mashindano hayo hatua ya makundi.

Tom Saintfiet alijiuzulu kama bosi wa Gambia dakika chache baada ya kuondolewa.

Kulikuwa na miondoko miwili ya ajabu wakati Algeria ilipoachana na Djamel Belmadi na Jalel Kadri kujiuzulu kama kocha wa Tunisia, lakini Ivory Coast pia ilichukua hatua ya haraka baada ya kumaliza nafasi ya tatu katika Kundi A.

Jean-Louis Gasset alilipa gharama ya mechi dhidi ya Equatorial Guinea, ambayo walifungwa mabao 4-0, lakini wakafuzu hatua ya mtoano kama timu nne washindwa bora (best looser) zilizomaliza nafasi ya tatu.

Wakati huo huo, Shirikisho la Soka Afrika limemfungia kocha wa Tanzania, Adel Amrouche. Kocha wa Morocco, Walid Regragui naye alifungiwa, lakini baadaye adhabu yake ikatenguliwa.

## Nukuu

"Nitaondoka Barcelona mwezi Juni. Tumefikia hatua ya kutorejea. Ni wakati wa mabadiliko. Nadhani ni wakati wa kuondoka. Nilizungumza na bodi na klabu leo [juzi]. Nitaondoka Juni 30. Nilichukua uamuzi huu siku zilizopita. Tayari nilijua. Lakini ni wakati wa kuiweka hadharani. Nafikiri wachezaji hawakuweza kujiweka huru. Sitaki kuwa tatizo kwa klabu, lakini kinyume," **Kocha wa Barcelona, Xavi Hernandez, baada ya kushuhudia timu yake ikipigwa mabao 5-3 na Villarreal pale Camp Nou juzi.**



"Bila shaka tunampenda. Kylian Mbappe ni mchezaji mzuri, ana nguvu na natarajia kumuona akicheza Saudi Arabia, katika timu yoyote kwenye michuano yetu. Saudi Arabia sasa ni kinara sokoni. Tuna Cristiano Ronaldo, Karim Benzema. Tuna michuano imara, na tutashangaza tena. Nyota zaidi watakuja. Saudi Arabia inapanga kuwa taifa namba moja katika soka. Hivi karibuni, " **Mwanamfalme Abdullah Saad Abdulaziz Al Saud wa Saudia**



"Hakuna klabu, hakuna nchi kwa mwaka ujao. Hakuna klabu nyingine ya Uingereza. Hata kama sina chakula, haitatokea," **Jurgen Klopp, kuhusu uwezekano wa kufundisha klabu ama timu ya taifa atakapoondoka Liverpool.**



Nipashe
Spotika





Straika mpya wa Simba, Freddy Kouablan (katikati), wakati akitumikia timu yake ya zamani ya Green Eagle

# NYOTA WANAOSUBIRIWA KWA HAMU NA MASHABIKI WA SOKA LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

KAMA mambo yataenda kama yalivyopangwa, katikati ya mwezi wa pili Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kuendelea tena baada ya kusimama kupisha michuano ya Kombe la Mapinduzi, na fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), inayoendelea nchini Ivory Coast.

Mashabiki wengi wa soka Tanzania wanasubiri kwa hamu urejeo wa ligi kama ulivyotangazwa na Bodi ya Ligi baada ya Taifa Stars kuondolewa AFCON, ambapo itatanguliwa kwanza na Kombe la FA.

Mashabiki wanaisubiri kwa hamu ligi kwa sababu mbalimbali, kwanza 'wameimisi', halafu wanataka kuangalia vyuma vilivyosajiliwa na klabu mbalimbali kipindi cha dirisha dogo la usajili kama yaliyomo yamo.

Kuna wachezaji wapya ambao watacheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza na wameimbwa sana kwenye kipindi hiki cha usajili. Wapo ambao wametoka klabu moja za Ligi Kuu kwenda nyingine, nao wanaangaliwa kama wanaweza kuleta tija walipohamia.

Ni kawaida kwa mashabiki wa soka nchini, kama wakifanya vema au vibaya watakuwa na cha kuzungumza.

Katika makala haya tunakuletea majina ya wachezaji nane ambao wanasubiriwa kwa hamu na mashabiki kuonekana dimbani, hawa hapa...

**1. Freddy Kouablan - Simba**

Ukiangalia kwa jicho la tatu na la kiufundi ni kama Freddy Michael Kouablan ndiye anaonekana atakuwa straika namba moja wa kikosi cha Simba.

Straika huyu mrefu aliyejaa misuli raia wa Ivory Coast, amesajiliwa kutoka Green Eagle ya Zambia na mpaka anatua Msimbazi ndiye kinara wa mabao nchini Zambia, akiwa na mabao 14 kwa mechi 16 alizocheza pamoja na 'asisti' nne katika Ligi Kuu ya huko.

Ametua kuziba pengo la mastraika tegemeo waliondoka, Moses Phiri na Jeen Baleke. Kama kuna mchezaji anayesubiriwa zaidi na mashabiki uwanjani, basi ni huyu.

**2. Joseph Guede - Yanga**

Tangu alipoondoka Fiston Mayele, Yanga inaonekana bado inatafuta straika wa kufanana naye. Pamoja na kumsajili Hafiz Konkoni raia wa Ghana, lakini bado hakuonekana kufiti kwenye eneo hilo.

Katikati ya ligi imekimbilia sokoni na kumleta Joseph Guede, raia wa Ivory Coast kutoka Tuzlaspor ya Uturuki. Mashabiki wanasubiri ligi ianze ili wamwangalie ni kweli anaweza kuvaa viatu vya Mayele, anakaribiana naye, au ndiyo yale kama ilivyokuwa kwa Konkoni.

**3. Franklin Navarro - Azam**

Alionekana kwenye mechi moja tu ya Kombe la Mapinduzi dhidi ya Chipukizi ya Zanzibar na wengi walionyesha kukoshwa na uwezo wake. Ndiyo kwanza alikuwa ametua kwenye kikosi akisajiliwa kipindi hiki kutoka Klabu ya Cortulua FC ya Daraja la Pili nchini kwao, Colombia.

Bahati mbaya Azam ilitolewa mapema, hivyo hakuonekana zaidi. Mashabiki sasa wanataka kumuona kwenye ligi na siyo tena Kombe la Mapinduzi.

Ikumbukwe hata Francy Kazadi aling'ara sana msimu uliopita na kuwa mfungaji bora kwenye michuano hiyo akiwa na Klabu ya Singida Fountain Gate akiwa ndiyo kwanza amesajiliwa na timu hiyo, lakini ligi ilipoanza akawa wa kawaida tu.

**4. Reliants Lusajo - Mashujaa FC**

Ameachana na timu yake iliyomtambulisha kwenye ulimwengu wa soka, akijiunga na Mashujaa FC yenye maskani yake mjini Kigoma.

Lusajo, mmoja wa mastraika bora wazawa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, pia ameshawahi kuitumikia kwa mafanikio Klabu ya KMC. Na hata alipoaga Namungo, baadhi walimhusisha kujiunga na timu kubwa kama Simba, Yanga, Azam FC na Singida Fountain Gate.

Ligi itakapoanza, mashabiki wana hamu ya kumuona kama ataendelea na uwezo wake ule ule wa kupachika mabao akiwa na timu hiyo mpya au la.

**5. Salim Aiyee - Coastal Union**

Amerejea tena kwenye Ligi Kuu, safari hii siyo kwenye Klabu ya Mwadui au KMC, ila ni Coastal Union. Straika huyu amejiunga na timu hiyo akitokea Mbuni FC ya Arusha. Ni mmoja wa wachezaji wachache kwenye dirisha hili aliyesajiliwa kutoka Ligi ya Championship kwenda Ligi Kuu Tanzania Bara.

Amesajiliwa Coastal akiwa tayari ameshapachika mabao tisa kwenye timu yake, akiwa mmoja wa wachezaji waliokuwa wakiwania kiatu cha dhahabu kwenye ligi hiyo.

Msimu wa 2018/19 ndiyo ulikuwa kilele cha mafanikio yake aliposhika nafasi ya pili kwenye ufungaji bora wa Ligi Kuu akimaliza na mabao 18 akiwa na timu ya Mwadui FC, chini ya Meddie Kagere wa Simba alikuwa kinara kwa mabao yake 23. Ligi itakapoanza mashabiki wanataka kuona kama ana kiwango kama kile cha mwanzo, au alitakiwa kubaki Championship.

**6. Omar Jobe - Simba**

Ni straika raia wa Gambia ambaye amesajiliwa na Simba kuchukua nafasi za kina Phiri na Baleke. Amesajiliwa kutoka Klabu ya Zhenis ya Kazakhstan ambapo mashabiki wengi si wa Simba tu, bali wa soka na Ligi Kuu ya Tanzania wanataka ligi ianze ili waone ni kweli alistahili kuja kuvaa viatu vya wachezaji hao au la.

**7. Augustine Okrah - Yanga**

Ni mchezaji ambaye mashabiki wa soka nchini wanamfahamu sana. Msimu uliopita aliichezea Klabu ya Simba na alianza akiwa na kiwango bora. Hata hivyo, kila muda ulivyokuwa unasonga mbele kiwango chake kilionekana kuporomoka.

Yakasemwa mengi kwa raia huyo wa Ghana kuwa ana tatizo la nidhamu nje ya uwanja, lakini pia majeraha yakatajwa kupunguza ubora wake.

Simba iliachana naye mwishoni mwa msimu, na akarejea kwenye klabu yake ya Benchem ya Ghana ambapo ghafla tu aliibuka na kurejea kwenye kiwango cha hali ya juu kabla ya kunyakuliwa na Yanga. Alicheza dakika chache kwenye mechi moja ya Kombe la Mapinduzu kabla ya kuumia.

Mashabiki wanataka ligi ianze wamuone kama atakuwa yule wanayemfahamu wakati anaingia Simba, au Okrah wa wakati anaachwa.

**8. Mohamed Mustafa - Azam**

Ni golikipa aliyetua Azam FC kwa mkopo wa miezi sita kutoka El Mereikh Omdurman ya Sudan. Anakumbukwa kuwa ndiye alikayekaa langoni katika mechi zote mbili ambazo timu hiyo ilicheza dhidi ya Yanga, Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu.

Ligi itakapoanza ndipo mashabiki watajua kama atachukua mikoba ya lundo la makipa waliokuwa kwenye kikosi hicho ambao viwango vya bado havijawavutua wapenzi wa klabu hiyo au na yeye ataanza vizuri kama wenzake na kuanza kufungwa mabao

**JE, WAJUA?**



MWANASOKA Bora wa Mwaka wa Afrika aliyetawazwa hivi karibuni, Victor Osimhen bado hajaweza kurejea katika kiwango kizuri alichopata alipofunga mabao mengi zaidi kwenye Serie A msimu uliopita na kuiwezesha Napoli kutwaa ubingwa, hata hivyo ana takwimu za juu zaidi za mabao yanayotarajiwa na majaribio ya kulenga lango kwenye fainali za Afcon, baada ya kupiga mashuti 13.





# Wanafunzi 120 warundikwa darasa moja

**Na Paul Mabeja,**
DODOMA

KIWANGO cha elimu kiko hatarini kushuka katika Shule ya Msingi Ntyuka ya jijini hapo kutokana na msongamano wa zaidi ya wanafunzi 120 kwenye darasa moja.

Mwalimu Mkuu msaidizi wa shule hiyo, Neema Masensi aliyasema hayo jana wakati akitoa taarifa kwenye ziara ya Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa Kata ya Ntyuka, Theobalt Maina, baada ya kukagua na kujionea kero zinazoikabili shule hiyo.

Mwalimu Masensi, alisema shule hiyo inakabiliwa na msongamano wa wanafunzi hali inayosababisha walimu kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Alisema kwa mujibu wa sera ya taifa ya elimu, kila darasa linatakiwa kuwa na wanafunzi kati ya 40 hadi 45 ili waweze kupata elimu bora.

"Shule yetu ina wanafunzi zaidi ya 1,800 inakabiliwa na tatizo la msongamano wa wanafunzi hali ambayo inachangia walimu kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo kwani darasa la wanafunzi 120 mwalimu hawezi kumpitia mtoto mmoja mmoja ili kukagua kazi yake na walimu walio ni 38," alisema.

Alisema kutokana na kukua kwa kasi kwa kata hiyo kumechangia ongezeko kubwa la watu na kuiomba serikali kusaidia ujenzi wa shule mpya ya Bwawani ili kuunga mkono juhudi za wananchi.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Bwawani Kata ya Ntyuka, Habel Mazengo, alisema kutokana na serikali kutoa elimu bure kumechangia miundombinu iliyopo kutotosheleza idadi ya wanafunzi.

"Tunaomba serikali itusaidie kupata shule nyingine ya msingi kwa kuwa shule mama imezidiwa na wanafunzi lakini ipo mbali hali ambayo imesababisha baadhi ya wanafunzi kushindwa kwenda shule kutokana na makolongo kujaa maji msimu huu wa mvua za masika," alisema Mazengo.

Kwa upande wake, Maina, alishauri Mwenyekiti wa Mtaa wa Bwawani kuwasiliana na Diwani wa Kata ya Ntyuka ili kukamilisha ujenzi wa shule mpya na kupunguza adha hiyo.

"Naomba wananchi waone umuhimu wa kuchangia ujenzi wa shule hii ya Bwawani ambayo itasaidia kupunguza msongamano katika shule mama ya Ntyuka wakati tunawasiliana na Mkurugenzi wa jiji kupata suluhu ya changamoto hii," alisema.



Naibu Mkurugenzi Idara ya Hijja na Umra BAKWATA Taifa, Omary Msenga, akizungumza na viongozi wa dini ya Kiislamu (hawapo pichani) katika Msikiti Mkuu wa Gadaff jijini Dodoma mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha kuwahamasisha waumini kuhusu safari ya kwenda kuhijji Makka mwaka huu. Wa pili kushoto ni Shehe wa Mkoa wa Dodoma, Mustaph Rajabu. **PICHA: PETER MKWAVIL**

# Wapewa mbinu kuepuka kausha damu

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

WAJASIRIAMALI wameshauriwa kuunda vikundi na kuvisajili ili kupata mikopo itakayowasaidia kukuza mitaji na kujiepusha na mikopo ya mitaani ya kausha damu na kuwadidimiza kiuchumi.

Ushauri huo ulitolewa jana na Diwani wa Kata ya Chamwino jijini hapa, Jumanne Ngede, wakati akifunga mafunzo ya utengenezaji wa bidhaa kwa wajasiriamali yaliyotolewa na Taasisi ya Star Entrepreneur General.

Alisema endapo wajasiriamali wakiungana watapata mikopo kutoka taasisi za kifedha zinazotambuliwa kisheria na yenye riba nafuu badala ya hiyo ya kausha damu ambayo inachangia umaskini ndani ya familia zao.

"Naomba nyinyi wajasiriamali ambao mmepata mafunzo haya kwa vitendo kwa kutengeneza bidhaa mbalimbali, muungane nendeni kwenye taasisi za kifedha zinazotambuliwa ikiwamo Halmashauri za Jiji mkakope fedha muendeshe biashara zenu kuliko kukimbilia kwenye hiyo mikopo ya chapuchapu ya kausha damu," alisema.

Diwani wa Viti Maalum, Rosemary Nitwa, aliwaasa kutumia elimu hiyo kurithisha familia zao ili vijana wao wajiajiri kupitia ujasiriamali.

Vilevile, aliwaasa kutumia elimu hiyo kutengeneza bidhaa zenye viwango ili kupata soko la uhakika la ndani na nje ya nchi.

Awali, Mkurugenzi wa Taasisi ya Star Entrepreneur General, Daniphord Kesaga, alisema wajasiriamali hao wamejifunza utengenezaji wa sabuni, kilimo, ufugaji, usindikaji wa karanga, batiki, chaki, mishumaa, usimamizi na ufuatiliaji wa masoko ndani na nje ya nchi.

# Tulia azungumzia mfumo utoaji haki mahakamani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk.Tulia Ackson amesema mfumo wa unukuzi na tafsiri katika mahakama 11 nchini utasaidia utoaji haki kwa wananchi kwa kuwa unatafsiri kutoka lugha ya Kiingereza na Kiswahili.

Dk.Tulia aliyasema hayo jana wakati akizindua Wiki ya Sheria iliyokwenda sambamba na maadhimisho ya mshikamano jijini hapa.

Alisema mfumo huo ambao umefungwa katika mahakama hizo nchini utakuwa na taarifa sahihi za kijamii kuhusu haki za binadamu nchini kwa sababu wananchi wengi wanategemea kupata haki zao mahakamani.

Alisisitiza kuwa ili mahakama ifanye kazi vizuri, inahitaji ushirikiano na taasisi nyingine ambazo nazo zinahitaji kwenda na kasi yake.

Dk. Tulia ameltaka Jeshi la Magereza, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Ofisi ya Mashtaka kuzipa Mahakama nchini ushirikiano wa kutosha ili jamii ipate haki kwa wakati.

"Mahakama imepiga hatua sana na taasisi nyingine shirikianeni nayo ili kuhakikisha haki za binadamu zinapatikana," alisema Dk. Tulia.

Awali Mtendaji Mkuu wa Mahakama hiyo, Profesa Elisante Ole Gabriel, alisema mfumo huo ambao unafanya kazi kama Roboti ya Kisayansi, utakuwa msaada katika utoaji haki za binadamu.

Prof. Gabriel, alisema mfumo huo kwa sasa unafanya kazi kwa asilimia 90 na kuwa na matokeo mazuri ya matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika uendeshaji wa kesi.

Alisema wanafanya utaratibu ili Tanzania iwe na haki ya umiliki wa mfumo huo ambao wameanza kuutumia katika baadhi ya Mahakama.

Aliitaja mikoani ambayo mfumo huo umefungwa kuwa ni pamoja na Dodoma, Arusha, Mwanza, Dar es Salaam na Kagera.

Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Profesa Ibrahim Juma, alisema kwa sasa teknolojia inashika kasi duniani ndio maana na wao wanatumia mfumo huo.

# Itigi kujenga miundombinu kwa bil. 6.4 /-

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Itigi mkoani Singida kwa mwaka wa fedha 2024/25 inatarajia kutumia Shilingi bilioni 6.4 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya afya na elimu.

Fedha hiyo ni kati ya Shilingi bilioni 19.975 zilizopitishwa na Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo kwa ajili ya bajeti ya mwaka huo wa fedha.

Akiwasilisha bajeti hiyo, Ofisa Mipango, Emmanuel Dyelu, alisema fedha hizo zitatumika kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari, majengo katika hospitali ya wilaya na nyumba za watumishi.

Dyelu alitaja baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23 ni ununuzi wa vishikwambi 20 kwa ajili ya uendeshaji wa vikao kidigitali, ujenzi wa nyumba ya mkurugenzi, usajili wa shule 25 za msingi, tatu za sekondari na ujenzi wa sekondari mpya ya Majengo.

Mengine ni ujenzi wa bweni la vyumba vya madarasa 10 vya sekondari, vyumba tisa vya madarasa katika shule kongwe za serikali.



# Waelimishwa kuepuka dawa za kulevya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UKOSEFU wa ajira kwa vijana katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini umetajwa kuwa chanzo cha baadhi yao kujiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya na kupoteza nguvu kazi ya taifa.

Ofisa Elimu wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini (DCEA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Adrick Ndelwa, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki iliyopita wakati akitoa elimu kwa viongozi wa Chama cha Waendesha Bajaji wa Jiji la Mbeya.

Ndelwa alisema kuwa utafiti wao umebaini kuwa watumiaji wengi wa dawa hizo ni vijana, hivyo mamlaka hiyo imeamua kuanza kutoa elimu kwa kundi hilo kupitia mikusanyiko na mikutano ya ndani na ya hadhara.

"Hii sekta imeajiri vijana wengi sana kwa hiyo sisi tumeona ni sehemu sahihi ya kutoa elimu kuhusu madhara ya matumizi ya dawa za kulevya, hapa wengi ni viongozi wa kanda na wamekiri walikuwa hawana elimu hii, kwa hiyo tunaamini watatusaidia kufikisha elimu kwa wenzao," alisema Ndelwa.

Aliwataka waathirika wa dawa hizo kutoa taarifa kwa mamlaka hiyo ili wapatiwe tiba saidizi na kurejee katika hali yao ya awali.

Mwenyekiti wa Waendesha Bajaj hao, Lucas Mwakyusa, aliwashukuru DCEA kwa kutoa elimu hiyo kwa sababu itasaidia kudhiditi matumizi ya dawa hizo katika jamii na kuwarejesha waathirika katika hali yao ya awali.

Alisema kwa kuwa kazi yao ni kusafirisha abiria, wanatakiwa kuwa na akili timamu ili kuepuka kusababisha ajali.

Alisema wengi wanaoendesha bajaji wanategemewa na familia zao na hivyo wanatakiwa wafanye kazi wakiwa katika hali ya usalama ili kuepuka kuziingiza familia zao kwenye matatizo.

"Mtu anayetumia dawa za kulevya anahama kabisa kwenye uhalisia wake wa kibinadamu, kwa hiyo anaweza akafanya vitu ambavyo siyo sahihi ikizingatiwa kwamba sisi tunasafirisha roho za watu, kundi letu lina vijana wengi tena wa kila rika hivyo elimu hii ni muhimu sana," alisema Mwakyusa.

Baadhi ya viongozi walioshiriki mafunzo hayo walikiri kuwapo kwa wenzao ambao wanatumia dawa za kulevya hasa bangi na hivyo wakaiomba DCEA kuendelea kutoa elimu hiyo.

Mmoja wa viongozi hao, Barick Sanga aliiomba mamlaka hiyo kuwadhibiti wasambazaji wa dawa za kulevya hasa zile zinazoingizwa nchini kutoka mataifa mengine duniani.

Alisema tatizo la bangi wanaweza kulishughulikia kupitia kwenye vyama vyao kwa kutumia sheria ikiwamo kuwafungia madereva wanaotumia dawa hizo.

"Kwa mfano watu kama sisi ambao tunatokea Uwanji, bangi ilikuwa inatumika kama mboga kabla serikali haijazuia, kwa hiyo hii ni rahisi kudhibiti, tunaomba mtusaidie kuwadhibiti hao wanaoleta maheroine na ma-cocaine kwa ndege kutoka nchi za mbali," alisema Sanga.

Dereva mstaafu wa bajaji, Steven Mwasomola, aliwaomba viongozi wa madereva hao kueneza elimu waliyoipata ili kila mmoja awe na uelewa wa kutosha na kuepuka kutumia dawa hizo.



Ofisa Elimu wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Adrick Ndelwa, akitoa elimu ya madhara ya dawa za kulevya kwa viongozi wa Chama cha Madereva wa Bajaji jijini Mbeya mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mwalimu mbaroni kwa ujambazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani hapa linawashikilia watu watatu akiwamo mwalimu wa Shule ya Msingi Mwaselela iliyopo Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, Azimio Gerlad (31) kwa tuhuma za ujambazi.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Benjamin Kuzaga, juzi aliwaambia waandishi wa habari kuwa watuhumiwa hao walikamatwa Januari 25, mwaka huu katika msako unaoendeshwa na jeshi hilo dhidi ya watu wanaojihusisha na vitendo vya uhalifu mkoani hapa.

Aliwataja watuhumiwa wengine kuwa ni Furaha Issa (32) na Goodluck Luben Mwakajisi (25) maarufu kwa jina la Kudu, wakazi wa Iwambi.

Alisema Mwalimu Azimio, mkazi wa Mtaa wa ZZK na watuhumiwa wenzake, walipopekuliwa walikutwa na mali za wizi, vifaa vya umeme, zana wanazotumia kuvunja nyumba na silaha za kuwatisha watu ili kufanikisha uporaji.

Alivitaja baadhi ya mali walizokutwa nazo watuhumiwa hao kuwa ni runinga, redio na spika zake, deki, kompyuta, chaja nane za kompyuta mpakato, simu, remoti na bidhaa za madukani.

Vilevile, alisema watuhumiwa hao walikamatwa na mashine ya kupimia shinikizo la damu hospitalini na nyingine ya kupimia damu.

Alisema watuhumiwa walikutwa na vifaa vya kuvunjia na kujeruhi watu ikiwamo mapanga, visu na vifaa vya kukatia milango ya chuma na makufuli.

Alisema baadhi ya mali zilizokamatwa zimetambuliwa na walioibiwa na akawataka wananchi wengine kwenda kuzitambua mali zao katika Kituo cha Polisi cha Mbalizi.

# 'Cheti za kuzaliwa hakimpi mtu uhalali wa uraia'

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Balozi Dk. Pindi Chana, amesema cheti cha kuzaliwa hakimpi mtu uhalali wa uraia bali ni uthibitisho wa kuzaliwa kwake.

Dk. Chana alitoa kauli hiyo baada ya kutembelea Ofisi ya Msajili wa Vizazi na Vifo (RITA) Mkoa wa Njombe kwa lengo la kuangalia hali ya uandikishaji na usajili wa watoto chini ya miaka mitano.

"Sio uthibitisho pekee na ndiyo maana cheti cha kuzaliwa hata mtoto ambaye wazazi wake wote wawili sio Watanzania ni wageni wamekuja kutalii akizaliwa Tanzania atapata cheti, hivyo katika vigezo vyetu vya kuangalia huyu ni Mtanzania ama sio, cheti cha kuzaliwa kinaweza kikatumika," alisema Dk. Chana.

Alisema cheti hicho kinathibitisha mtu huyo ni mzaliwa nchini Tanzania, lakini si hakikisho la mwisho kuwa ni mzawa.

"Tukija kwenye utaratibu wa uraia kuna taratibu zake, kuna sheria zake za kutambua huyu je ni Mtanzania au sio Mtanzania, hivyo niwakumbushe cheti cha kuzaliwa kinaonyesha mtoto amezaliwa wapi na habari za uraia kuna taratibu nyingine," alisema.

Dk. Chana, alisema kila mtoto Mtanzania anapozaliwa anayo haki ya kupata cheti cha kuzaliwa kwa sababu ni haki ya kila mmoja.

"Watanzania wenzangu, wamama hivi sasa tupige marufuku kabisa watu kujifungulia nyumbani, watu wanatakiwa kujifungulia katika vituo vya afya ili mpate vyeti vya kuzaliwa vya watoto," alisema.

Kwa upande mwingine, amewaagiza wakurugenzi wa halmashauri nchini kutenga fedha kwa ajili ya usajili wa watoto chini ya miaka mitano.

Awali Mratibu wa RITA Mkoa wa Njombe, Rahabu Daud, alisema mpango wa usajili wa watoto chini ya miaka mitano katika mkoa huo ulianza Septemba mwaka 2016.

Daudi alisema tangu kuanza kwa mpango huo hadi Januari 25, mwaka huu, watoto 190,075 wamesajiliwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa.

Alisema takwimu hizo zinaonyesha kuwa kiwango cha usajili katika mkoa huo kimeongezeka kutoka asilimia 8.6 (sensa 2012) hadi kufikia asilimia 64.9 mwaka huu.

Alisema kabla ya kutekeleza mpango huo, Halmashauri za Wilaya za Njombe, Ludewa na Wanging'ombe hali ya usajili ilikuwa asilimia sita mwaka 2012 na kuongezeka hadi asilimia 65 Januari mwaka huu.



## Waziri aagiza wapangaji ZHC wachukuliwe hatua

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Rahma Kassim Ali, amewataka wapangaji wa nyumba za Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC) kufuata sheria na kuagiza waliokiuka kuchukuliwa hatua kali.

Rahma alitoa rai hiyo wakati akizungumza na wananchi na wakazi wa nyumba za Mombasa Kwamchina visiwani hapa kwenye kikao kilichoandaliwa na uongozi wa shirika hilo.

Alisema nyumba hizo zina masharti na miongozo ambayo imeainishwa katika mikataba, hivyo kila mmoja anatakiwa kuzingatia.

Alisema miongoni mwa mambo yasiyoruhusiwa katika nyumba hizo kuwa ni mpangaji kuzungusha uzio wa maturubali, makuti, kufungua gereji na sehemu za kuoshea magari.

Rahma aliuomba uongozi wa Manispaa ya Mjini na Jiji kuchukua hatua kwa wapangaji waliobadilisha matumizi ya maeneo hayo kwa kufanya kazi zisizoruhusiwa ikiwamo kufungua maegesho na maduka ya kuuza magari.

Mkurugenzi Mkuu wa ZHC, Mwanaisha Ali Said, aliwataka wapangaji wa nyumba hizo kulipa kodi ili fedha zitakazopatikana zitumike kuzifanyia ukarabati nyumba hizo kwa wakati.

Vilevile aliwataka wapangaji hao kutoa kufaya usafi katika maeneo yanayowazunguka badala ya kusubiri kazi hiyo kufanywa na shirika.

Vilevile, alipiga marufuku wapangaji hao kupaka rangi nyumba kila mmoja anayopenda bila ya maelekezo kutoka kwa uongozi wa shirika kwa vile nyumba hizo zinatakiwa kuwa katika mwonekano wa aina moja.

Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Makazi, Hannat Bakar Hamad, alitoa wito kwa wananchi kujitokeza na kuunda jumuiya na kufanya usajili ili kutatua changamoto zinazowakabili wananchi.

Alisema uwepo wa jumuiya hizo kutasaidia uanzishwaji wa sheria na kanuni za kuweka usalama wa watu na makazi yao.

Wakitoa maoni yao, wapangaji hao, walilalamikia uvamizi katika maeneo hayo kwa kufanya kazi zisizoruhusiwa na kuzua hofu miongoni mwao hasa kwa watoto wao.

Ali Khamis, aliutaka uongozi wa shirika hilo kulipatia ufumbuzi tatizo la kutuama kwa maji taka katika makazi yao ili kunusuru kutokea kwa milipuko ya magonjwa na mazalia ya mbu.

# Wizara yajitosa kuinusuru ZECO

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Nchi, Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar, imesema imeandaa mkakati wa kulilipa Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) madeni ya taasisi za serikali ili liweze kujiendesha kwa ufanisi zaidi.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Juma Malik Akil, alitangaza mpango huo mwishoni mwa wiki iliyopita wakati akizungumza na makatibu wakuu wa wakurugenzi wa taasisi na mashirika ya umma visiwani hapa.

Alisema maofisa masuuli wanapaswa kufahamu madeni yatakayolipwa hayatokani na fedha za mfuko mkuu bali ni za matumizi ya kawaida za taasisi ambazo zitakatwa moja kwa moja na kupelekwa ZECO kwa ajili ya kulipa deni hilo.

Alisema serikali imekuwa ikipokea madeni mengi ya umeme kutoka kwa shirika hilo na kusababisha kushindwa kusimama na kujiendesha kutokana na kutolipwa madeni hayo na taasisi hizo za serikali.

Alisema ni lazima kusimamia ulipaji madeni kwa ZECO na kwa utaratibu kwamba maofisa masuuli wawe wanatenga bajeti kulipa madeni hautawezekana.

"Sitaki kutaja nani na nani anadaiwa, lakini kuna deni kubwa hili nataka tulifahamu kuna kiasi cha pesa kuanzia sasa tutaanza kulipa moja kwa moja ZECO kwa taasisi zinazodaiwa," alisema Dk. Akil.

Akizungumzia sekta ya nishati, alisema pamoja na kufanya vizuri katika miundombinu ya barabara na minngine, kwa upande wa nishati bado hawajaifanyia kazi ipasavyo.

Dk. Akil alizitaja baadhi ya changamoto zinazopelekea kuchelewa kwa fedha za maendeleo kuwa ni makubaliano ya utekelezaji wa miradi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Ali Suleiman Mrembo, aliwataka watendaji wa serikali kutekeleza majukumu yao ili kuhakikisha uchumi unazidi kuimarika na huduma bora zinaendelea kupatikana.

Mrembo alisema ili kukuza uchumi ni lazima kuwapo mazingira mazuri na wezeshi na sekta binafsi na za umma kuwajibika ipasavyo kutoa huduma bora.

Alisisitiza kuangalia vyanzo vinavyotokana na mapato yasiyokuwa ya kodi ili kuzinusuru wizara kubeba jukumu hilo.

Alizitaka taasisi za serikali kutumia ipasavyo kwa kile ambacho wamekipanga na kukienzi na kuhakikisha wanatumia mifumo ya kielektroniki kupata mapato ya serikali kwa ufanisi mkubwa.



Naibu Katibu wa Habari, Uenezi na Uhusiano kwa Umma, Janeth Rithe, akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana kuhusu maazimio mbalimbali ya Kamati Kuu iliyokutana jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Zanzibar kuimarisha mifumo ya ununuzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI Mtendaji Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA), Othman Juma Othman, amesema kuimarishwa kwa mifumo ya manunuzi kutaongeza ufanisi kwa watendaji wa serikali na kwenda sambamba na mifumo ya dunia.

Othman aliyasema hayo jana wakati akifungua warsha ya mapitio ya mfumo wa manunuzi (MAP) iliyowashirikisha watendaji wa taasisi zinazohusika na manunuzi Zanzibar.

Alisema dunia imekuwa ikitumia mifumo maalum ya manunuzi, hivyo kuna haja kwa maofisa manunuzi nchini kutumia hasa kwa taasisi za serikali ili kuondoa kasoro zinazojitokeza wakati wa kununua vifaa vya taasisi za serikali. Aliwataka maofisa hao kuboresha utendaji kazi wakati wanapofanya manunuzi kwa maslahi ya umma na taifa.

Akizungumzia kuhusu changamoto iliyopo kwenye manunuzi, Othman, alisema inachelewesha ununuzi wa vifaa vya serikali hasa ukizingatia kuwa inaendelea kujenga majengo ya huduma mbalimbali visiwani hapa.

Msimamizi wa manunuzi ukanda wa mashariki na kusini mwa Afrika ambaye anawakilisha Benki ya Dunia (WB), Ishtiak Siddigue, alisema benki hiyo iko tayari kusaidia Tanzania kufanya mifumo ya manunuzi ili kupunguza mapungufu yanayojitokeza na kuleta mafanikio katika ununuzi wa mali za umma.

Alisema benki hiyo itaangalia ajenda ya manunuzi kwenye mifumo inayotumiwa na nchi zilizoendelea ili ilingane na ya dunia.

Mtaalamu wa manunuzi WB, Raymond Mbishi, aliwataka washiriki kuangalia mapungufu ya manunuzi kwa kufuata mifumo ya dunia kwenye taasisi za umma.

Washiriki wa warsha hiyo waliahidi kubadilika katika kufanya manunuzi na kuishukuru benki hiyo kuandaa mkutano huo Zanzibar.

# Wananchi watakiwa kujitokeza kujua dalili za ugonjwa wa ukoma

**Na Steven William, MUHEZA**

MRATIBU wa kifua kikuu na ukoma wilayani Muheza, Jessie Ewald, amewataka wananchi wilayani hapa kutambua kuwa ugonjwa wa ukoma bado upo, wanapaswa kujitokeza kupima afya zao mapema wanapoona dalili.

Wito huo aliutoa jana kwenye maadhimisho ya Siku ya Ukoma Duniani wakati wa utoaji wa elimu kwa jamii ya ugonjwa huo, baada ya kuwatembelea wagonjwa wa ukoma majumbani kuwapa elimu.

Alisema lengo la utoaji wa elimu hiyo ni wananchi watambue kuwa ugonjwa huo upo wilayani kwao.

Akizungumzia hali kwa sasa ya ugonjwa huo, alisema wagonjwa bado wanaendelea kuwapo, mwaka jana 25 waligundulika kuwa na ugonjwa huo.

Hata hivyo, alisema kwa kushirikiana na Shirika la GRL, wameshaanza kufanya utafiti kwa maeneo mbalimbali ya Muheza ili kujua watu wenye ugonjwa huo na kutibiwa mapema.

Mwenyekiti wa watoa huduma ngazi ya jamii wilaya hiyo, Zakaria Mhina, aliwataka wananchi wanapoona dalili za ugonjwa wa ukoma kufika katika Hospitali ya Teule Muheza, watibiwe.

Aliwataka wananchi kupima afya zao kwa kuwa maradhi ya ukoma ni hatari na yanatibika.

Muuguzi kitengo cha kifua kikuu na ukoma katika hospitali hiyo, Andrew Kalimbe, aliwataka wananchi kufahamu kuwa ugonjwa wa ukoma upo na ni maradhi hatari zaidi, wanapaswa kwenda hospitali wanapoona dalili mapema za ugonjwa huo.

Mgonjwa wa ukoma mkazi wa Kwamkabara, Salimu Juma aliyetembelewa kupewa elimu, alisema ameugua ugonjwa wa ukoma kwa miaka 10 sasa.

Alisema kuwa alipopatwa na ugonjwa huo alijua amelogwa, lakini baadaye alipata ushauri na kufika hospitali na kuambiwa kuwa ana ugonjwa wa ukoma na kuanza matibabu na sasa anatumia dawa anaendelea vizuri.

Alisema ameoa mke na kuzaa naye watoto watatu ameishi naye miaka 21, lakini baada ya kupata ugonjwa huo mke wake aliondoka nyumbani.

Juma alisema kuwa ugonjwa huo upo, anaomba serikali ifuatilie kwa karibu ili uweze kutokomezwa na kuwajali wagonjwa kwa kupatiwa dawa bure.

Alisema kuwa anawashauri wananchi ambao wamepata ugonjwa huo wa ukoma waende hospitali kwani ukoma sio ugonjwa wa kulogwa.



Mwenyekiti wa Watoa Huduma Ngazi ya Jamii Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Zakaria Mhina (wa pili kulia), akimpatia kipeperushi Salimu Juma, kinachohusu ufahamu wa dalili za ugonjwa wa ukoma katika maadhimisho ya Siku ya Ukoma Duniani jana. Kulia ni Mratibu wa Kifua Kikuu na Ukoma, Jessie Ewald na Muuguzi Kitengo cha Kifua Kikuu na Ukoma Hospitali Teule ya Muheza, Andrew Kalimbe. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Zaidi ya bil. 1/- zaidhinishwa kujengwa barabara

**Gideon Mwakanosya, RUVUMA**

WAKALA wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) wilayani Namtumbo, mkoani Ruvuma imeidhinishiwa kutumia Sh. bilioni 1.1 kutoka Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa ajili ya matengenezo ya barabara na utawala.

Akitoa taarifa kwenye kikao cha kamati ya ushauri wilayani humo (DCC) kwa niaba ya Meneja wa TARURA, Mhandisi Albert Mtimba, alisema zaidi ya Shilingi bilioni moja zimeidhinishwa kutumika katika mwaka wa fedha wa 2023/2024.

Mtimba alisema fedha hizo zitatumika kuhudumia mtandao wa barabara wenye jumla ya kilomita 975.254 na madaraja 74.

Aidha, Mhandisi Mtimba alifafanua kuwa katika kilomita 975.254, kilomita 4.603 ni barabara za lami sawa na asilimia 0.47 na kilomita 280.369 barabara za changarawe.

Mhandisi Mtimba alisema kilomita 690.281 ni barabara za udongo Wilaya ya Namtumbo..

Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, akiwamo Diwani wa Kata ya Litola, Paulo Kamilius Fussi, walihoji kitendo cha utengenezaji wa barabara wakati wa masika na kusababisha usumbufu kwa watumiaji.

Alisisitiza umuhimu wa kuweka kifusi katika barabara zinazotengenezwa na kuziacha bila kuweka kifusi kinasababisha kutopitika wakati wa mvua kutokana na utelezi.

Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la Wilaya ya Namtumbo, Ngollo Malenya, pamoja na mambo mengine aliwataka wakuu wa taasisi, wakuu wa idara na vitengo kuzingatia maoni na ushauri uliotolewa na wajumbe wa baraza katika taarifa zao na kuwaagiza maoni na ushauri huo ukafanyiwe kazi.

# Morogoro yajipanga kuwa kitovu uzalishaji viungo

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

MKOA wa Morogoro umejipanga kuwa ni sehemu ya kitovu cha uzalishaji wa mazao ya viungo ikiwamo karafuu kutokana na sehemu ya ardhi katika mkoa huo kuonyesha uzalishaji wenye tija wa kilimo cha zao hilo.

Mpango huo wa Serikali ya Mkoa wa Morogoro umelenga kuwaongezea wigo wakulima kuchagua mazao ya biashara ili kuongeza kipato cha wananchi, mkoa na taifa kwa ujumla.

Katibu Tawala mkoa huo, Dk. Mussa Ali Mussa, alisema mkakati huo licha ya kuwa ni kitovu cha uzalishaji wa mazao hayo pia unalenga uhifadhi na utunzaji wa mazingira kwa kurejesha uoto wa asili ikiwamo kwenye safu ya milima Uluguru.

Dk. Mussa alisema hayo wakati wa kikao cha watendaji wa Wizara ya Kilimo cha kutambulisha mradi wa uzalishaji wa miche ya mikarafuu kwa ajili ya wakulima wa halmashauri za mkoa huo.

Alisema kwa kushirikiana na mashirika mengine yakiwamo Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), watatoa bure kwa wananchi miche ya mazao ya viungo ikiwamo ya karafuu.

Alisema hatua hiyo ni mpango mkakati wa utunzaji miti ambayo ni rafiki kwa maji pamoja na binadamu kwa kuwapatia tija na kuacha kukata miti na kuharibu mazingira ikiwa na kusaidia kutunza uoto wa asili kwenye vyanzo vya maji na milima ya Uluguru.

Dk. Mussa alisema, wananchi hasa wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro wamehamasika na kuanza kupanda miche ya karafuu na kuzalisha vitalu vya miche hiyo 400,000 na mkoa umejipanga kuinunua na kuigawa kwa wengine kuipanda.

Katika hatua nyingine alisema, mkoa huo umeanza kujenga maghala ya kuhifadhia karafuu ili kuwa na sehemu moja ya kuuzia zao hilo hasa katika halmashauri hiyo.

Dk. Mussa alisema kujengwa kwa maghala hayo kutaisaidia halmashauri hiyo kusimamia vyema ukusanyaji mapato yake vizuri kupitia mazao ya kilimo yakiwamo ya viungo.

Mkurugenzi Msaidizi wa Uzalishaji wa Mazao, Wizara ya Kilimo, Beatrice Banzi, alisema lengo la kikao hicho inatokana na utafiti uliofanywa na wizara hiyo siku za nyuma baada ya Mkoa wa Morogoro kuonesha nia ya kulima zao hilo.

Alisema wizara ilifanya utafiti na kugundua kuwa sehemu kubwa ya Mkoa wa Morogoro inaweza kustawisha zao la karafuu na kuongeza kipato cha wananchi na kuhifadhi mazingira kwa sababu miti yake haifyonzi maji.

Alisema katika utekelezaji wa azma hiyo, wizara imetafuta miche 235,000 ya mikarafuu kwa ajili ya kupandwa katika Halmashauri za Mkoa wa Morogoro na kazi ya uoteshaji wa miche hiyo imepewa TARI Mlingano, mkoani Tanga.

Alisema, kabla ya kupewa miche hiyo baadhi ya wakulima na viongozi watapelekwa kupata mafunzo ya siku tatu katika kituo hicho ili kupewa ujuzi wa kustawisha zao hilo na baada ya mafunzo hayo watapewa miche hiyo tayari kwa kupandwa.

Katibu Tawala Msaidizi sehemu ya uchumi na uzalishaji mali, Dk. Rozalia Rwegasira alisema, watahakikisha wanatekeleza maono ya mkoa kustawisha mazao ya viungo ikiwamo karafuu na mpango huo umepewa jina la Morogoro Spice Aroma Hub ikiwa na kurudisha uoto wa asili wa Milima ya Uluguru.

HABARIKIMATAIFA



Wafanyakazi wa UNRWA wakiongoza moja ya magari yanayopeleka misaada Ukanda wa Gaza. **PICHA: MTANDAO**

# Maofisa wa UNRWA watuhumiwa kushiriki shambulio la Hamas

**GAZA, Palestina**

MATAIFA kadhaa duniani yametangaza kusitisha ufadhili wake kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuwahudumia Wakimbizi wa Kipalestina (UNRWA) baada ya wafanyakazi wake kadhaa kutuhumiwa kuhusika na shambulizi la Oktoba 7, 2023.

Ilielezwa kuwa mataifa hayo ikiwamo Finland, Italia, Canada na Australia ni mojawapo ambayo hivi karibuni yalitangaza kusitisha msaada wote wa kifedha kwa UNRWA.

Ilielezwa kuwa hatua hiyo inafuatia hatua ya Marekani ambayo juzi pia ilitangaza kusitisha ufadhili wote kwa UNRWA. Huku Uingereza nayo ikisema inasitisha sehemu ya ufadhili wake kwenye shirika hilo.

Ilibainishwa kwamba tuhuma zinazolikabili shirika hilo ni kuwa wafanyakazi wake 12 wanahisiwa kushiriki katika kutekeleza shambulizi la kundi la Hamas dhidi ya Israel, jambo linalotajwa kuwa chanzo cha vita vinavyoendelea Ukanda wa Gaza.

Ilielezwa kuwa Marekani ilijibu tuhuma hizo kwa kutangaza mara moja kusitisha ufadhili wote wa kifedha kwa UNRWA.

UNRWA ilisema juzi kuwa imewafukuza kazi wafanyakazi wake kadhaa waliotuhumiwa na Israel kushiriki shambulizi la Hamas kwa taifa hilo.

Mkuu wa shirika hilo, Philippe Lazzarini, aliahidi kwamba atawachukulia hatua wote ikiwa ni pamoja na kuwashtaki kwa kosa la jinai, mfanyakazi yeyote atakayebainika kujihusisha na matendo ya kigaidi.

Inaelezwa kuwa uamuzi huo utakuwa pigo kwa juhudi za msaada zinazotolewa kwa Palestina hasa wakati huu wa vita kati ya Israel na wapiganaji wa Hamas.

UCHUNGUZI WASISITIZWA

Wakati huo huo, Waziri wa Mambo ya Nje wa Australi, Penny Wong, alisema kuwa amestushwa mno na madai yaliyotolewa dhidi ya UNRWA.

"Tunazungumza na washirika na kwa muda tutasitisha fedha tulizopanga kuzitoa hivi karibuni," aliandika Wong kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa X.

Mwanadiplomasia huyo wa Australia pia alisema wanazikaribisha hatua zilizochukuliwa na UNRWA ikiwamo uamuzi wa kusitisha mikataba na tangazo lake la kuanzisha uchunguzi kamili wa madai hayo dhidi ya shirika hilo.

Aidha, Canada kupitia Waziri wa Maendeleo ya Kimataifa, Ahmed Hussein, ilisema serikali mjini Ottawa imesitisha kwa muda msaada ziada kwa UNRWA kupisha uchunguzi wa tuhuma zinazotolewa.

Alisema Canada inazichukulia tuhuma hizo kwa uzito mkubwa na kwamba inashirikiana kwa karibu na UNRWA na wafadhili wengine kutafuta mzizi wa jambo hilo.

Canada pia imelitolea mwito shirika hilo la Umoja wa Mataifa kuchukua hatua nzito haraka iwezekanavyo iwapo itathibitika miongoni mwa wafanyakazi wake walishiriki hujuma dhidi ya Israel Oktoba 7.

Kufuatia uamuzi wa mataifa kusitisha ufadhili wake, serikali ya Mamlaka ya Ndani ya Palestina imetoa rai kwa jumuiya ya kimataifa kutowatupa mkono watu wa Palestina na kwamba UNRWA inahitaji msaada mkubwa.

Waziri wa Ustawi wa Jamii wa Palestina, Hussein Al-Sheikh, aliandika kupitia ukurasa wa mtandao wa X kuwa Palestina inahitaji msaada badala ya kuondolewa misaada.

Israel kwa upande wake iliapa kwamba Shirika hilo la Umoja wa Mataifa halitoendelea na kazi yake Ukanda wa Gaza baada ya vita kumalizika. Na kwamba itafanya kila liwezekenalo kusitisha shughuli zake.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa mahusiano kati ya pande hizo mbili yamezorota katika siku za karibuni baada ya UNRWA kusema kombora lililofyatuliwa na kifaru limeipiga moja ya kambi za watu waliopoteza makazi huku kwenye mji wa kusini mwa Gaza wa Khan Younis.

Vile vile, kundi la Hamas linatajwa kuishambulia Israel kwa kile vimekiita vitisho vya nchi hiyo dhidi ya Shirika la UNRWA.

Kundi hilo linalotawala Ukanda wa Gaza limeitaka Jumuiya ya Kimataifa kutohadaika na vitisho na ulaghai wa Israel.

**DW**

## UN Afrika yabariki uamuzi wa ICJ dhidi ya Israel

**UN, Afrika**

MWENYEKITI wa Tume ya Umoja wa Mataifa Afrika, Moussa Faki Mahamat, amekaribisha uamuzi wa Mahakama ya Kimataifa ya Haki (ICJ), ambayo iliitaka Israel kuzuia kitendo chochote kinachowezekana cha mauaji ya kimbari huko Gaza.

Katika taarifa iliyotolewa jana mwenyekiti huyo alisema uamuzi huo unathibitisha kuheshimiwa kwa sheria za kimataifa na hitaji la Israel kufuata ipasavyo majukumu yake chini ya Mkataba wa Mauaji ya Kimbari.

Ilielezwa kuwa Mahakama ya Kimataifa ya Haki mjini Hague ilitoa uamuzi wake wa kwanza juzi katika kesi hiyo ya kihistoria kwa mpango wa Afrika Kusini, ambaye ni mwanachama wa Umoja wa Afrika.

Mahakama hiyo alisema Israel lazima ichukue hatua zote katika uwezo wake wa kuzuia kitendo chochote cha mauaji ya kimbari na kwamba hakuna kiongozi anayepaswa kutoa matamshi ya kuchochea mauaji ya halaiki.

"Taifa la Israel lazima lichukue hatua madhubuti mara moja ili kuwezesha utoaji wa huduma za kimsingi na misaada ya kibinadamu," ilisema ICJ.

Afrika Kusini iliishutumu Israel kwa kukiuka Mkataba wa Mauaji ya Kimbari wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 1948 uliaonzishwa baada ya Vita vya Pili vya Dunia na Holocaust wakati wa kampeni yake ya kijeshi huko Gaza, iliyoanzishwa na Hamas katika ardhi ya Israel mnamo Oktoba 7, 2023.

Ilielezwa kuwa mahakama haikutoa uamuzi iwapo Israel ilikuwa ikifanya mauaji ya halaiki. Na kwamba ilitoa maagizo ya dharura kabla ya kukagua kesi hiyo kwa uhalali wake, mchakato unaotarajiwa kuchukua miaka kadhaa. Huku Mahamat akisema Umoja wa Afrika umekaribisha hatua zilizoamriwa na mahakama.

Vita huko Gaza vilianza na shambulio la Hamas mnamo Oktoba 7, ambalo lilisababisha vifo vya watu 1,140 nchini Israel, wengi wao wakiwa raia, kwa mujibu wa hesabu ya shirika la habari la AFP likijikita kwa takwimu rasmi za Israel.

Wanamgambo hao pia walichukua karibu mateka 250 na Israel inasema karibu 132 kati yao wamesalia Gaza, ikiwa ni pamoja na miili ya mateka 28 walioaga dunia.

Israel iliapa kuiangamiza Hamas na kuanzisha mashambulizi ya kijeshi ambayo, kwa mujibu wa wizara ya afya ya Gaza, imesababisha vifo vya watu 26,257, wengi wao wakiwa wanawake, watoto na vijana.

**VOA**

# NBC YAAHIDI MAKUBWA ZAIDI MASHINDANO WAITARA TROPHY

**Na Mwandishi Wetu**

MASHINDANO ya Gofu ya 'NBC Waitara Trophy 2024' yamehitimishwa kwa mafanikio makubwa huku mdhamini mkuu wa mashindano hayo, benki ya NBC, ikiahidi kuendelea kuyaboresha zaidi ili yaendelea kuwa chachu ya kukuza na kuendeleza vipaji vya mchezo wa gofu, kutangaza utalii sambamba na kumuenzi mwasisi wa michuano hiyo Mkuu wa Majeshi Mstaafu, Jenerali George Waitara.

Katika mashindano hayo yaliyohitimishwa na mwasisi wake Jenerali Waitara kwenye viwanja vya Klabu ya Gofu vya Lugalo, Dar es Salaam jana, yalihusisha washiriki takriban 122 kutoka ndani na nje ya nchi, ikishuhudiwa wachezaji wa Klabu ya Gofu Lugalo waking'ara zaidi huku mchezaji Boniface Japhet kutoka klabu hiyo akiibuka mshindi wa jumla.

Akizungumza kwenye hafla ya kukabidhi zawadi kwa washindi mbalimbali wa mashindano hayo, Jenerali Waitara pamoja na kuwapongeza washiriki na wadhamini, alitoa wito kwa jamii kushiriki kwa wingi kwenye mchezo huo unaojiongezea umaarufu hapa nchini huku akiwasihi wapuuzie dhana iliyojengeka kwa muda mrefu kuwa mchezo wa gofu ni mahususi tu kwa watu wenye kipato kikubwa kwenye jamii.

"Niwasihi sana wazazi mwendelee kuwaruhusu watoto na vijana wenu wajitokeze kwa wingi kushiriki mchezo huu kwa kuwa mbali na sababu za kiafya pia umekuwa ukiambatana na fursa mbalimbali za kiuchumi kwa washiriki huku pia ukitoa wasaa kwa washiriki kukutana na watu wa aina mbalimbali ndani na nje ya nchi hatua ambayo imekuwa ikiwasaidia kufungua fursa mbalimbali za kijamii na kibiashara," alisema.

Zaidi Jenerali Waitara alitoa wito kwa wadhamini wa mashindano mbalimbali ya mchezo huo ikiwa ni pamoja na kuangalia namna ya kupanua udhamini wao, pia waone namna ya kuboresha viwanja vya mchezo huo husus an kwenye mfumo wa umwagiliaji ili viweze kuwa katika hali nzuri hata msimu wa ukame.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Idara ya Wateja Wadogo na Binafsi wa NBC, Elibariki Masuke, Mkuu wa Idara ya Bima, Benki ya NBC, Benjamin Nkaka, alisema ushiriki wa benki hiyo kwenye mashindano hayo kwa kiasi kikubwa unasukumwa na adhma ya benki hiyo katika kukuza na kuendeleza sekta ya michezo nchini ili kuibua vipaji, kuchochea ajira kupitia michezo pamoja na kuitumia vema sekta hiyo katika kutangaza utalii wa ndani.

"Kwetu mchezo wa gofu tunautazama kama moja ya michezo ya kimkakati inayoweza kulitangaza zaidi taifa hili huku pia ukitoa fursa kwa makundi tofauti ya wanajamii kuweza kujijengea fursa tofauti zikiwamo zile za kiuchumi bila kujali umri, jinsia au daraja lolote kiuchumi. Tumeamua kuunga mkono jitihada za muasisi wa mashindano haya Jenerali Waitara tukitambua hilo. Tunaahidi kuendeleza uhusiano wetu huu mzuri kupitia mashindano haya ili yaweze kutimiza malengo ya kuanzishwa kwake," alisema Nkaka.

Akizungumzia mashindano hayo, Meneja wa Klabu ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania ya Lugalo-(JWTZ), Kanali David Mziray, alisema licha ya kufanyika kwa mafanikio imeshuhudiwa washiriki mbalimbali wakiwamo watoto wakifanya vizuri zaidi kwenye mashindano hayo kwa kupata alama nzuri zaidi hatua ambayo inawahakikishia ujio wa vipaji bora zaidi katika wakati mfupi ujao.

"Kupitia mashindano haya tumeshuhudia watoto wakifanya vema zaidi kwenye baadhi ya maeneo kiasi ambacho alama zao zinatoa changamoto kwa wakubwa hususan kwenye eneo kama upigaji wa mipira mirefu, hatua ambayo inatuonyesha mwanga mzuri huko tuendapo. Katika kuhakikisha hili linafanikiwa klabu yetu ya Lugalo tunatoa mafunzo ya mchezo wa gofu kwa watoto bure katika siku zote za Jumamosi," alibainisha.

Kwa upande wao Rais wa Chama cha Gofu Tanzania (TGU), Gilman Kasiga na Rais wa Chama cha Gofu cha Wanawake Tanzania (TLGU), Queen Siraki, pamoja na kuonyesha kuvutiwa kwao na mafanikio makubwa ya mashindano hayo yanayoboreshwa kila mwaka walivutiwa zaidi na ongezeko kubwa la ushiriki wa wanawake na watoto kwenye mashindano hayo hatua ambayo walisema inathibitisha mwamko wa wana jamii katika kuupokea mchezo huo.




Mkuu wa Majeshi Mstaafu na Mwasisi wa Mashindano ya Gofu ya NBC Waitara Trophy, Jenerali George Waitara (wa pili kulia), akikabidhi zawadi ya kikombe na fedha taslimu kwa mshindi wa jumla wa mashindano hayo, Boniface Japhet, kutoka Klabu ya Gofu ya Lugalo jana Dar es Salaam. Wanaoshuhudia ni Mkuu wa Idara ya Bima Benki ya NBC, Benjamin Nkaka (wa tatu kushoto), Rais wa Chama cha Gofu cha Wanawake Tanzania (TLGU), Queen Siraki (kushoto) na Meneja wa Klabu ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania ya Lugalo (JWTZ), Kanali David Mziray (kulia). **MPIGAPICHA WETU**

# Shikangwa arejea upya na 'hat-trick'

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa timu ya soka la Wanawake ya Simba Queens, Jentrix Shikangwa, juzi alipiga 'hat-trick' yake ya kwanza akiwa ndiyo kwanza amerejea kwenye kikosi hicho, akitokea Klabu ya Beijing Beikong Women ya nchini China.

Shikangwa aliiongoza Simba Queens kupata ushindi wa mabao 7-0 dhidi ya Alliance Queens katika mechi ya Ligi Kuu ya Soka Wanawake iliyochezwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Alipachika mabao hayo dakika ya 48, 77 na 80, huku mengine yakifungwa na Asha Djafar aliyefunga mawili, Vivian Corazone na Aisha Mnunka.

Shikangwa raia wa Kenya, alikuwa mfungaji bora kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita kabla ya kupigwa bei nchini China kwa miezi sita kwenda kuichezea timu hiyo iliyo kwenye Ligi Kuu nchini humo, lakini sasa amerejea akiwa amesajiliwa kipindi cha dirisha dogo la usajili lililomalizika Januari 15, mwaka huu.

Hii ni 'hat-trick' ya pili kwenye Ligi Kuu ya Wanawake kwani nyingine ilitupiwa pia na mchezaji wa Simba Queens, Mnunka, aliyefunga mabao yote matatu Janauri 16, wakishinda 3-2 dhidi ya Amani Queens.

Bao la Mnunka pia linamfanya kufikisha mabao tisa, sasa akiwa sawa na Stumai Abdallah wa JKT Queens ambao msimu huu wanaonekana kufukuzana kukisaka kiatu cha dhahabu, ingawa wanaweza kupata wakati mgumu baada ya Shikangwa kurejea.

"Ni matokeo ambayo tuliyakosa wiki iliyopita kule Mara, tukatoka suluhu dhidi ya Bunda Queens na baada ya hapo tukawa tumejiwekea mipango kuwa tuhakikishe leo tunashinda mabao mengi ili tusijiweke mbali sana kwenye eneo la mabao ya kufunga na kufungwa dhidi ya mpinzani wetu mkubwa, JKT Queens," alisema Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally.

Matokeo mengine ya ligi hiyo wiki hii, Ceassiaa Queens iliitungua Baobab Queens mabao 2-0, mechi ikichezwa Uwanja wa Samora Iringa, Yanga Princess ikishinda bao 1-0 dhidi ya Bunda Queens.

## Mashujaa yatia fora dirisha dogo

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mashujaa FC ya Kigoma, imeweka rekodi ya kusajili wachezaji wengi kipindi cha dirisha dogo la usajili ikiwa imeingiza wachezaji saba kwenye kikosi chake mpaka sasa.

Mashujaa ambayo imeweka kambi yake jijini Dar es Salaam kujiandaa na mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara zitazoanza kuchezwa tena katikati ya mwezi Februari baada ya kusimama kutokana na fainali za AFCON, imeonekana kufanya usajili wa wachezaji wengi kipindi hiki ili kurudisha moto iliyokuwa nao kipindi ipo Ligi ya Championship na mechi za kwanza baada ya kupanda.

Timu hiyo imewasajili wachezaji Nyeyezi Juma kutoka Inter Star ya Burundi, Emmanuel Mtumbuka (Stand United) inayocheza Ligi ya Championship, Mpoki Mwakinyuke, Samson Madeleke, Omari Abdallah (Prisons), Reliants Lusajo (Namungo) na golikipa Patrick Muntari.

Kocha Mkuu wa Mashujaa FC, Mohammed Abdallah 'Bares', amesema kuwa usajili wote umefanyika kwa manufaa ya klabu, hasa baada ya kuangalia mapungufu yaliyojitokeza kwenye mechi ambazo tayari wameshacheza.

## KenGold yavutwa shati Championship

**Na Adam Fungamwango**

VINARA wa Ligi ya Championship, KenGold FC, juzi walivutwa shati na kupunguzwa kasi yao ya kuelekea kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara, walipolazimishwa suluhu dhidi ya Mbeya Kwanza katika mechi kali ya raundi ya 19, iliyochezwa Uwanja wa Sokoine, jijini Mbeya.

Matokeo hayo yanatishia uongozi wa timu hiyo kwenye msimamo wa ligi kwani imefikisha alama 43, nyuma ya Pamba FC yenye pointi 40 na ina mchezo mmoja dhidi ya Biashara United ambapo kama ikishinda inaweza kukaa juu ya msimamo wa ligi hiyo kwa tofauti nzuri ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Suluhu hiyo inaipeleka Mbeya Kwanza nafasi ya sita ya msimamo ikiwa na pointi 36 ikipigania nafasi ya kupanda Ligi Kuu angalau kwa kucheza mechi za 'play off.'

Wakati KenGold ikipata ikizuiwa wiki hii, TMA ya Arusha iliachia kipigo cha mabao 3-0 dhidi ya Pan African, mechi ikichezwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### OLISE ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA ina nia ya kumsajili Michael Olise wa Crystal Palace msimu huu majira ya baridi, lakini winga huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 22, anapendelea kuhamia Manchester United. **(Football. London)**

### MRITHI WA KLOPP ASAKWA

LIVERPOOL itakabiliana na kibarua kigumu cha kupata kocha wanaoyemlenga ili kuchukua mikoba ya Jurgen Klopp msimu huu, huku Xabi Alonso akifuatiliwa na Bayern Munich na Roberto de Zerbi wa Brighton akilengwa na Manchester United iwapo watamfuta kazi Erik ten Hag. **(Telegraph)**

### ALONSO KUBAKI LEVERKUSEN

BAYER Leverkusen wana uhakika Xavi Alonso atasalia katika klabu hiyo msimu huu licha ya klabu yake ya zamani ya Liverpool kumtaka. **(Sky Germany)**

### BENRAHMA AFIKIRIWA EVERTON

KLABU ya Everton inafikiria kumnunua kwa mkopo winga wa West Ham na Algeria, Said Benrahma, mwenye umri wa miaka 28. **(HITC)**

### ESTEVE AWINDWA BURNLEY

KLABU ya Burnley imetoa dau la pauni milioni 10.2 kumnunua beki wa kati wa Montpellier mwenye umri wa miaka 21, raia wa Ufaransa, Maxime Esteve. **(Mail)**

### ROWE AWANIWA WEST HAM

IWAPO Said Benrahma ataondoka mwezi huu basi West Ham wanaweza kutafuta mpango wa kumnunua winga wa Norwich mwenye umri wa miaka 20, Jonathan Rowe. **(Talksport)**

### CHOLOBAH ATAKIWA FOREST

KLABU za Nottingham Forest, West Ham na Fulham zinafikiria kumnunua beki wa Chelsea mwenye umri wa miaka 24, Trevoh Chalobah. **(Football Insider)**

### ROBERTS SASA AGOMBEWA

KLABU za Brentford, Feyenoord na Leeds United zinavutiwa na beki wa kulia wa Burnley, Conor Roberts mwenye umri wa miaka 28. **(Mail)**

### HOJBJERG AIVUTIA LYON

KLABU ya Lyon bado inavutiwa na kiungo wa kati wa Tottenham Hotspur na Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg mwenye umri wa miaka 28 na mshambuliaji wa Villarreal , Arnaut Danjuma (26), ambaye yuko kwa mkopo Everton. **(L'Equipe)**

### SENSI KWA MKOPO LEICESTER

LEICESTER City imetoa ofa ya kumsajili kiungo wa kati wa Inter Milan, Stefano Sensi mwenye umri wa miaka 28 kwa mkopo na chaguo la kufanya uhamisho huo kuwa wa kudumu. **(Gianluca di Marzio)**


### ALMINOR ANYATIWA SAUDIA

KLABU ya Saudi Arabia ya Al-Shabab bado inavutiwa na winga wa Newcastle United mwenye umri wa miaka 29 kutoka Paraguay, Miguel Almiron. **(Mail)**

### RONALDO AKARIBIA SWANSEA

KLABU ya Swansea inakaribia kumsajili winga wa Brazil mwenye umri wa miaka 27, Ronald kutoka Gremio Anapolis. **(Wales Online)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# VAN DIJK: NI NGUMU KUKUBALI KLOPP ANAONDOKA LIVERPOOL

●●● Sote tunataka kufikia mengi na mawazo hayo yalikuwa tayari tangu kabla ya msimu mpya...

**LIVERPOOL, England**

VIRGIL van Dijk amesema uamuzi wa kocha Jurgen Klopp kujiuzulu kama kocha wa Liverpool mwishoni mwa msimu huu ni „mgumu kuukubali".

Klopp wa Ujerumani alitangaza Ijumaa kwamba ataacha jukumu lake kama kocha Julai mwaka huu.

Aliitaarifu klabu kuhusu uamuzi wake mnamo Novemba mwaka jana, lakini wachezaji waliambiwa muda mfupi kabla ya tangazo la umma la Ijumaa.

„Kocha ana maana kubwa kwetu, kwangu na kwa klabu," alisema nahodha huyo wa ‚Wekundu' hao, Van Dijk.

„Lakini alifanya uamuzi kwa ajili yake na familia yake. Siku zote ilikuwa ngumu na hakika ilikuwa hivyo.

„Alituambia faragha bila shaka na sisi sote tulikuwa pamoja. Ni ngumu kuchukua lakini mawazo yetu ni kuzingatia biashara. Tuna malengo mengi ya kufikia mwaka huu na kwa nini tusimalize msimu kwa kasi pamoja na sherehe za bosi pia?"

Van Dijk alijiunga na Liverpool katikati ya msimu wa tatu wa Klopp katika klabu hiyo na ameshinda tuzo kuu sita pamoja na kocha huyo mwenye umri wa miaka 56.

Wekundu hao bado wako kwenye mashindano manne, wakiwa wamejikatia tiketi ya kucheza fainali ya Kombe la Carabao dhidi ya Chelsea kwa kuifunga Fulham.

„Sote tunataka kufikia mengi na mawazo hayo yalikuwa tayari tangu kabla ya msimu mpya na hiyo haibadiliki," alisema Van Dijk mwenye umri wa miaka 32.

„Labda itakuongezea nguvu ya kufanya ziada hiyo au labda kufurahia zaidi pamoja na kufanya sehemu ya mwisho ya msimu - muda wa mwisho wa kocha katika klabu - wakati bora zaidi kuwahi kuwa nao.

„Hilo ndilo tunalojitahidi na ndiyo sababu ni biashara kama kawaida."

# LOOKMAN: ATOA SIRI NIGERIA KUFUZU ROBO FAINALI AFCON

**ABIDJAN, Ivory Coast**

ADEMOLA Lookman amesema juhudi za pamoja za wachezaji wenzake wa Nigeria ndizo zilizofanikisha ushindi wa 'Super Eagles' wa mabao 2-0 dhidi ya Cameroon ambao uliwasaidia kutinga Robo Fainali ya michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika, Afcon, Jumamosi.

Lookman aliifunga mabao mawili Nigeria ilipoilaza Cameroon kwenye Uwanja wa Felix Houphouet-Boigny mjini Abidjan na kutinga robo fainali hiyo.

Lookman, ambaye alitajwa kuwa mchezaji bora wa mechi hiyo, alisema: "Wow, tuna furaha sana kufuzu robo fainali.

"Tunapocheza pamoja zaidi, ndivyo tunavyozidi kuwa wazuri. Nimesimama hapa sasa, lakini tuzo hii inaakisi utendaji wa timu nzima."

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, anafurahia uzoefu wake wa kwanza wa michuano ya Afcon: "Ninapenda hali hii, ni ya ajabu. Usiku wa leo (juzi) mashabiki wetu walitusukuma hadi mwisho kwa sababu hii tukaishinda Cameroon, na unapovaa jezi ya Super Eagles, baadhi ya michezo inasikika zaidi."

Ijumaa wiki hiii, Nigeria itacheza na Angola katika mechi ya robo fainali, baada ya 'Swala Weusi' hao kuwafunga Namibia mabao 3-0 katika mchezo wa mapema Jumamosi.

Lookman aliongeza: "Angola ni timu nzuri. Tutaichambua na kujiandaa. Kadri unavyozidi kwenda ndivyo inavyokuwa ngumu ndivyo tutakavyochukulia mchezo baada ya mchezo."

Nigeria inatafuta taji lake la nne na la kwanza katika michuano hiyo tangu mwaka 2013.




## Angola ilistahili kufuzu – Dala

**ABIDJAN, Ivory Coast**

MSHAMBULIAJI wa Angola, Jacinto Dala, amesema walistahili kufuzu Robo Fainali ya michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon), inayoendelea nchini Ivory Coast.

Angola maarufu kama Swala Weusi hawakuzuilika dhidi ya Namibia walipowalaza mabao 3-0, huku Jacinto Dala akihusika katika mabao yote matatu.

Fowadi huyo aliishia kushinda tuzo ya mchezaji bora wa mchezo kwa kiwango chake bora, ambapo ni mara ya pili anaitwa kwenye michuano hiyo.

Dala alipongeza kiwango cha wachezaji wenzake na kuashiria kuwa walistahili kufuzu robo fainali hiyo.

"Tulikuwa na uchezaji mzuri sana leo (juzi). Timu hii ilistahili kufuzu na nina furaha sana tulifanya hivyo. Nitasema kujitolea na ushiriki wa wachezaji wote ulinisaidia kushinda mchezaji bora wa mechi," alisema.

Mabao hayo mawili yanamaanisha kuwa Jacinto Dala sasa amefunga manne kwenye michuano hiyo na sasa amepitwa bao moja tu na Emilio Nsue wa Equatorial Guinea mwenye mabao matano.

"Kufunga mabao hapa kunanifurahisha na ningependa kuendelea kufunga katika mashindano haya na kupata ushindi pia," aliongeza.

# Xavi kujiuzulu Barcelona Julai

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernandez ametangaza kuwa ataondoka katika klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu baada ya kichapo cha mabao 5-3 Jumamosi kutoka kwa Villarreal kwenye Uwanja wa Cam Nou.

Presha ilikuwa ikiongezeka kwa Xavi Januari yote baada ya msururu wa matokeo mabaya, ikiwa ni pamoja na kufungwa 4-1 na Real Madrid kwenye fainali ya Supercopa ya Hispania na kipigo cha 4-2 Jumatano kutoka kwa Athletic Club katika robo fainali ya Copa del Rey.

Xavi, ambaye hivi karibuni alisaini mkataba mpya hadi 2025, amesema alifanya uamuzi huo kabla ya mechi ya Villarreal, lakini huo ndio wakati muafaka kutangaza rasmi.

"Ningependa kutangaza kwamba sitasalia kuwa kocha wa Barca baada ya msimu huu," alisema Xavi katika mkutano na waandishi wa habari.

"Nilikuwa nimeamua kuondoka siku chache zilizopita, lakini nadhani sasa ni wakati muafaka wa kutangaza ili kusaidia kupunguza mvutano uliopo kwenye klabu na mabadiliko ya nguvu yanahitajika.

"Kwa hiyo, kama shabiki wa Barca, nikifikiria maslahi ya klabu, na wachezaji, nadhani ni uamuzi sahihi. Hakuna aliye mkubwa kuliko klabu na mimi ni mfuasi zaidi ya yote. Naipenda klabu hii."

Kufungwa na Villarreal kumeiacha Barca na pointi 10 nyuma ya vinara wa LaLiga, Real Madrid.

Kipigo cha Jumamosi kilikuwa mara ya kwanza kwa Barca kuruhusu mabao matano kwenye mechi ya nyumbani ya LaLiga tangu Januari mwaka 1963, walipochapwa mabao 5-1 na Real Madrid.

Pia ni mara ya kwanza tangu mwaka 1951 kufungwa mabao manne au zaidi katika mechi mfululizo.

Wamebakia kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku wakiwakabili Napoli katika mechi mbili katika hatua ya 16 bora mwezi ujao, na Xavi bado ana matumaini ya kufanya vizuri huko.

"Nitatoa zaidi katika miezi hii iliyobaki," aliongeza. "Bado nadhani tunaweza kubadilisha mambo na kuwa na msimu mzuri. Nadhani tunaweza kupigania LaLiga, hata tukiwa nyuma kwa pointi 10.

"Nadhani tangazo hili linaweza kuwakomboa wachezaji na kusaidia kupunguza mvutano katika klabu. Hawastahili lolote - ni kundi kubwa. Kwa namna fulani limenikomboa mimi pia.

"Sitaki kuwa tatizo kwa klabu, nataka kuwa suluhu. Nilikuwa suluhu miaka miwili iliyopita nilipoteuliwa, lakini sasa nikifikiria kwa moyo wangu na kuifikiria klabu, ni bora kuondoka katika majira ya joto."

Xavi amesisitiza uamuzi wake "hauwezi kubadilishwa" hata kama atapata mafanikio makubwa kwa kipindi cha msimu kilichobaki.

"Hisia ya kuwa kocha wa Barca inaweza kuwa mbaya," aliendelea. "Ni ukatili, kuna ukosefu wa heshima kwako, kazi yako haithaminiwi ... ni mbaya kwa afya yako ya akili na ari yako.

"Mimi ni mtu mzuri, lakini inafikia wakati unafikiri hakuna maana ya kuendelea. Ndivyo ilivyo."

Aliongeza kuwa bado hajawasilisha uamuzi huo kwa wachezaji wake kwa sababu walikuwa "wamechanganyikiwa" kwenye chumba cha kubadilishia nguo baada ya mechi ya Villarreal, lakini atazungumza nao kwenye mazoezi Jumapili.

HABARI MICHEZO

# MWAKINYO AMCHAPA MGHANA KWA KO SASA AMTAKA KIDUKU

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

BAADA ya Bondia wa Ngumi za Kulipwa nchini, Hassan Mwakinyo, kushinda Mkanda wa Ubingwa wa WBO Afrika, kwa kumchapa Mghana Elvis Ahorgah kwa KO katika raundi ya saba kwenye pambano la raundi 10 uzani wa Super Middle, lililopigwa Indoor New Amaan Sports Complex mjini Zanzibar usiku wa kuamkia jana, amesema sasa anamtaka Twaha Kiduku ulingoni ili kumaliza ubishi dhidi yao.

Mwakinyo ameshinda pambano hilo huku akiweka rekodi za kushinda mkanda wa ubingwa huo kwa mara ya kwanza ambao umekuwa ni ndoto yake ya muda mrefu.

Haikuwa rahisi kwa Mwakinyo kupata ushindi huo kwani alipata wakati mgumu kwenye raundi mbili za mwanzo ambapo mpinzani wake alionekana yuko fiti zaidi.

Mwakinyo alianza kuwanyanyua vitini mashabiki kuanzia raundi ya nne, alipoonekana ni kama amemsoma mpinzani wake kiasi cha kutomhofia tena na kuanza kumpelekea makonde kadhaa ambayo taratibu yalianza kumnyong'onyesha Mghana huyo.

Ilipofika raundi ya saba, Mghana huyo alijichanganya na kutaka kumvurumishia makonde Mwakinyo, lakini aliacha mwanya ambao Mwakinyo aliutumia kumaliza mchezo kwa kumchapa makonde mawili ya haraka yaliyomfanya kuanguka chini na baadaye kushindwa kuendelea na pambano.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwakinyo alisema ushindi wake ni salamu tosha kwa bondia wa Morogoro ,Twaha Kiduku' kwani amekuwa akipiga kelele muda mrefu kutaka kupigana naye, hivyo amewataka mapromota kuweka mkwanja wa kutosha ili weweze kumaliza ubishi wao.

„Kwanza namshukuru Mungu kwa kuweza kushinda ubingwa huu, lakini niwashukuru mashabiki wangu kwa kuonyesha imani kubwa juu yangu licha ya kukosa nafasi kwa kipindi kirefu, lakini wameweza kunivumilia wakati wote huo hadi leo hii nikionyesha kile ambacho naamini nimejaliwa kuwa nacho.

„Lakini ushindi huu nataka uwe Salamu tosha kwa yule bondia wao wa Morogoro ambaye wanasema namwogopa, nipo tayari kupanda naye ulingoni wakati wowote kitu cha msingi ni kwa promota kuzingatia suala la fedha tu na siyo jambo lingine, nataka nikatoe fundisho ili wengine waache kufikiria kwa urahisi," alisema Mwakinyo.

Kwa upande wa Promota wa pambano hilo kutoka Peak Time Media Production, Selemani Semunyu, alisema amefurahishwa na mwitikio ulioonyeshwa na wadau wa mchezo wa ngumi visiwani Zanzibar.

„Nikiwa kama mzoefu wa mchezo wa ngumi, nimeona kitu cha tofauti baada ya mamia ya watu kujitokeza kwa wingi na kujaza meza zote mapema kitu ambacho kimenipa faraja kubwa," alisema Semunyu.

Aidha, alimpongeza Mwakinyo kutokana na kiwango alichokionyesha katika pambano hilo na kudai mabondia wengi Tanzania watanufaika na mkanda huo.

WATANI WA JADI...



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Azania, Esther Mang'enya, akikabidhi medali ya ushindi kwa Mbunge Tunza Malapo, wakati wa mashindano ya Bunge Bonanza yaliyofanyika jana katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma na kudhaminiwa na benki hiyo. Mashindano hayo yaliwakutanisha wabunge na watumishi wa Bunge wanaoshabikia timu za Yanga na Simba. Kulia ni Spika wa Bunge, Tulia Ackson, ambaye alikuwa mgeni rasmi. **MPIGAPICHA WETU**

# Serengeti Girls yataka kufanya kweli Zambia

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Timu ya Taifa ya Wasichana cha chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), kinachonolewa na Bakari Shime, kipo tayari kwa ajili ya kuwakabili Zambia katika mchezo wa kuwania kufuzu Kombe la Dunia.

Serengeti Girls inaendelea na kambi katika Kituo cha Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), kilichopo Kigamboni kwa ajili ya mchezo huo utakaochezwa Februari 2, mwaka huu, nchini Zambia na baadaye kurudiana Tanzania katika Uwanja wa Azam Complex.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Shime alisema licha ya kutopata muda wa kucheza mechi ya kirafiki kujiandaa na mchezo huo kutokana na muda, kikosi chake kipo tayari kukabiliana na wenyeji wao, Zambia katika mechi hiyo.

Alisema anatambua hautakuwa mchezo rahisi, lakini kulingana na mazoezi wanayofanya anaimani kubwa vijana hao wataenda kufanya vizuri katika mchezo huo wa ugenini.

"Licha ya kutopata mechi za kirafiki kutokana na ratiba kubana, tunaendelea na maandalizi mazuri na tunatarajia kufanya vizuri katika mchezo wetu huo wa kwanza ugenini na baadaye tutarudia nyumbani," alisema Shime.

Kikosi cha nyota hao kinaundwa na makipa; Marian Shaban, Mwanaidi Maulid (Bunda Queens) na Salome Saint (Geita Gold Queens), mabeki ni Sarah Joel, Manka Richard (Fountain Gate Princess), Neema Damas (Baobab Queens), Edna Makamba (Oysterbay Queens), Ladia Maximilian (JKT Queens), Masika Mwakisua (Yanga Princess), Sarah Lucas na Kurwa Rockets (Bunda Queens).

Viungo ni Winifred John (Yanga Princess), Ester Maseke, Melikia William, Semeni Juma (Bunda Queens), Naomi Charles, Sabina Alex, Asha Ramadhani (Geita Gold Queens) na Marry Siyame (Laliga Academy- Spain) na Washambuliaji ni Jamil Rajabu, Yasinta Mitoga, Winifrida Gerald, Mwantima Mwarabu (Geita Gold Queens) na Jamil Celestine (Bunda Queens).

## Gamondi hataki kuacha kitu Yanga

INATOKA UK. 24

Kombe la Mapinduzi iliyofanyika mjini Zanzibar na kushuhudia Mlandege ikitwaa tena ubingwa kwa mara ya pili, ikiifunga Simba bao 1-0.

Itakuwa wiki tano tangu ilipocheza mechi ya mwisho ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Desemba 23, mwaka jana, kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma dhidi ya Tabora United, ikishinda bao 1-0, ambapo kuanzia hapo haijacheza mechi yoyote Bara.

Tayari, wachezaji Maxi Nzengeli na Clement Mzize wameshatoa yao ya moyoni kuhusu 'kuwamisi' mashabiki wa soka kutokana na kukaa muda mrefu bila kucheza.

Walisema wanawakumbuka mashabiki wa timu hiyo jinsi wanavyokuwa nao kila wanapokwenda na wanavyowashangilia kitu ambacho kinawapa moyo wa kupamba kwa ajili yao, hivyo wana hamu ya kuwaona tena.

Ratiba inaonyesha kuwa baada ya hapo, Yanga inatarajiwa kushuka dimbani kwa mara ya kwanza katika mechi ya Ligi Kuu, Februari 16, kucheza dhidi ya JKT Tanzania.

## Benchikha kutumia Tembo kutesti straika

INATOKA UK. 24

nyota muhimu ambao wako kwenye majukumu ya timu za taifa na wengine kujiunga hivi karibuni baada ya kutolewa lakini haitaathiri mipango ya mbinu zake kuelekea mchezo huo wa FA.

"Kuna baadhi ya wachezaji hawakuwapo kwenye maandalizi ya mechi yetu ijayo, tulioanza nao wanajua umuhimu wa mchezo huo, mabadiliko yatakuwapo madogo kwa sababu ya kuwapa nafasi nyota wapya, lakini tukichanganya na wale waliopo mwanzo.

"Ninapambana kwa moyo wote kwa ajili ya kushinda kila siku, Simba tupo kwenye michuano ya CAF ambayo nataka tufike mbali zaidi ya matarajio ya wengi, lakini ubingwa wa ligi ni muhimu lazina tufanye vizuri tushinde," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa yupo Simba kuendelea kufanya kazi yake kwa jitihada zote kuhakikisha wanaendeleza furaha kwa mashabiki wao na kufikia kile ambacho kinatararajiwa na Wanasimba katika kila mechi iliyopo mbele yao.

Kuhusu nyota wapya, alisema anategemea kuwapa nafasi katika mechi dhidi ya Tembo akitumia mchezo huo kutafuta matokeo mazuri pamoja na kupata muunganiko wa wachezaji wapya na waliokuwapo tangu awali.

Naye Meneja Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema kuanzia leo au kesho baadhi ya wachezaji waliokuwapo kwenye timu za taifa watajiunga na wenzao kwa ajili ya kujiandaa na mechi zijazo za ligi na michuano ya kimataifa.

Michezo
Jumatatu Januari 29, 2024
Nipashe

Van Dijk: Ni ngumu kukubali Klopp anaondoka Liverpool UKURASA 21






Mshambuliaji wa Nigeria, Ademola Lookman, akishangilia sambamba na straika mwenza, Victor Osimhen, baada ya kuifungia mabao yote mawili wakati ikishinda 2-0 dhidi ya Cameroon kwenye mechi ya hatua ya 16-bora ya michuano ya Afcon iliyopigwa Uwanja wa Felix Houphouet-Boigny, Ivory Coast juzi. Kwa matokeo hayo Nigeria sasa imetinga robo fainali. **PICHA: MTANDAO**

# GAMONDI HATAKI KUACHA KITU YANGA

●●●Apania makombe yote akianzia Housing FC Kombe la FA kesho, asema ni safari ya Ligi ya Mabingwa na...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema wanakwenda kucheza mechi ya Kombe la FA dhidi Housing FC ya Njombe kesho Jumanne kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, ili kujiweka sawa na mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika na Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kocha huyo ambaye yuko na kikosi hicho kwa wiki mbili sasa akikifua kuanzia kwenye ufukwe wa Coco na baadaye uwanjani, amesema ni muhimu kushinda mechi hiyo kwa sababu ni moja kati ya makombe makubwa Tanzania, lakini itawafanya wachezaji wake kujiamini zaidi, hivyo atautumia mchezo huo kama mazoezi ili kupima kikosi chake kama



kimesharejea kwenye mtiririko na kasi anayoitaka kwa ajili ya michuano mingine.

"Tunakwenda kucheza mechi ya FA, tunajiandaa kushinda mechi hii kwa sababu itaturejesha kwenye morali, pia hatutaki kulipoteza kombe hili, lakini ni mchezo ambao kila mchezaji anatakiwa aonyeshe kuwa amerudi kwenye kiwango chake kile cha mwanzo au zaidi kwa sababu ni kama mazoezi kuelekea Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema kocha huyo.

Alisema hadhani kama wachezaji waliokuwa kwenye kikosi cha timu ya taifa watacheza mechi hiyo kwa sababu watakuwa wamechelewa na watahitaji wapumzike, badala yake wachezaji atakaowatumia wengine wao ni wale alioanza nao mazoezi.

Yanga itacheza mechi ya kwanza baada ya wiki tatu kupita tangu ilipotolewa kwenye hatua ya robo fainali ya

INAENDELEA UK. 23



# Benchikha kutumia Tembo kutesti straika

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha ameahidi kufanya mabadiliko ya kikosi cha timu hiyo katika mchezo wa Kombe la Shirikisho (FA Cup) dhidi ya Tembo FC utakaochezwa Jumatano hii katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Mabadiliko hayo ni baada ya baadhi ya nyota wake waliokuwa kwenye majukumu ya timu zao za Taifa katika Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon), nchini Ivory Coast, ambapo kwa Tanzania ni Aishi Manula, Mohammed Hussein 'Tshabalala', Mzamiru Yassin na Kibu Denis, huku kwa Zambia akiwa Clatous Chama ambao wanatarajiwa kujiunga na timu yao kuanzia leo baada ya kutolewa katika hatua ya makundi.

Hata hivyo, ataendelea kumkosa beki kisiki cha 'Wekundu wa Msimbazi' hao, Enock Inonga Baka, ambaye timu yao ya Taifa ya DR Congo, imetinga hatua ya 16 bora ya fainali hizo zinazoendelea nchini Ivory Coast.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha huyo alisema anategemea kufanya mabadiliko ya kikosi chake kuelekea katika mchezo wao ujao wa FA dhidi ya Tembo ambao utamsaidia kuandaa kikosi rasmi kwa ajili ya michezo iliyopo mbele yao, Ligi Kuu Tanzania Bara na Ligi ya Mabingwa Afrika.

Alisema licha ya kutokuwapo kwa

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >